BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,012,798,111/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**ACT-Wazalendo yaibuka na hoja tano za wananchi, imo uhaba ajira**



**UNITED YAONGEZA OFA KWA MARTINEZ**

UKURASA 21

Jumamosi Julai 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581001

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# CCM: Msimchukulie poa Rais Samia

**HOJA ZA CAG**
Wengi wanawajibishwa kimyakimya



**MACHINGA KURUDI**
Tathmini imefanywa, ripoti iko mezani

**KATIBA MPYA**
Chama kimeamua kuwasikiliza wananchi

**TUME HURU**
Kikosi Kazi kitatoa mwelekeo wa muundo wake

UKURASA 4



Rais Samia Suluhu Hassan na Shaka Hamdu Shaka

# Kesi kina Mdee ngoma ngumu, CHADEMA wajipanga upya

UKURASA 2



Halima Mdee



Freeman Mbowe.

## Wafanyabiashara 6 Kariakoo kortini mashtaka kukwepa kulipa kodi bil. 8.6/-

UKURASA 2

MICHEZO MCHENGERWA ANG'AKA YANGA IKITAWALA TUZO UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Kesi ya kina Mdee bado ngoma ngumu

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Masjala Kuu imetoa kibali kuwaruhusu Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, na wenzake 18 kufungua kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama wa CHADEMA baada ya kukubaliana na hoja tano za waleta maombi.

Vilevile, imewapa siku 14 Mdee na wenzake kufungua kesi hiyo kama sheria inavyoelekeza, huku viongozi wa chama hicho wakisisitiza wanawasubiri wapambane mahakamani.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Mustapha Ismail wa mahakama hiyo baada ya kupitia hoja tano za kisheria za waleta maombi (Mdee na wenzake), wajibu maombi (CHADEMA) na maoni ya Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola.

Jaji Ismail alisema amekubaliana na hoja zote tano za waleta maombi kwamba maombi hayo yalifunguliwa ndani ya muda wa kisheria.

Alisema maombi waliyofungua, yanaonesha kuna jambo linalobishaniwa na pia yameonyesha kuwapo maslahi mapana ya waleta maombi.

Pia alisema waleta maombi walitafuta haki zao ndani ya CHADEMA.

Mdee na wenzake walifungua kesi hiyo dhidi ya Baraza la Wadhamini la CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

**NJE YA MAHAKAMA**

Wakili wa CHADEMA, Peter Kibatala, alisema wanakubaliana na uamuzi wa mahakama na hawana mpango wa kukata rufani kwa kuwa watawanufaisha waleta maombi.

Wakili wa Waleta maombi, Edson Kilatu, alisema wanasubiri kupata nakala ya uamuzi huo ili kuanza mchakato wa kufungua kesi mapema.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema hawajakubaliana na uamuzi wa mahakama hiyo kwa kile alichodai siyo uamuzi wa haki.

Alisema kwa kuwa hawawezi kukata rufani kwa hatua hiyo, watapambana katika hatua zijazo kutafuta haki.

Alisema wapo tayari kuendelea na mapambano hadi haki ipatikane kwa kuwa kisheria kutakuwa na muda usiozidi siku 90 wa kusikiliza kesi hiyo na wanaamini haki itapatikana.



Mhariri wa Gazeti la Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago (kulia), akifafanua jambo kwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alipotembelea ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga. **Picha zaidi uk. 7. PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafanyabiashara Kariakoo kortini mashtaka kukwepa kodi bil. 8.6/-

**Na Grace Gurisha**

WAFANYABIASHARA sita wa Kariakoo Dar es Salaam wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka saba ya ukwepaji kodi na kuisababishia Mamlaka ya Mapato (TRA) hasara ya Sh. bilioni 8.6.

Washtakiwa hao ni wafanyabiashara Ibrahim Magenge (32), mkazi wa Kijichi; Eliyasau Mohamed (29), mkazi wa Buza; Elisha Numvile (29), mkazi wa Mtoni kwa Azizi Ali; Juma Samatta (47), mkazi wa Kigogo na Siraji Mtungule (32), mkazi wa Makongo Juu na Ofisa Mauzo.

Akisoma hati ya mashitaka, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Emmanuel Medalakini, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ritha Tarimo, kuwa washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya ukwepaji kodi, matumizi yasiyo sahihi ya mashine za kielektroniki (EFD) na kusababisha hasara.

Medalakini alidai kati ya Januari na Juni 29, 2022 maeneo ya Kariakoo, Ilala Dar es Salaam kwa pamoja walitoa risiti ya uongo kwa kwa kutumia mashine ya kielektroniki ya EFD iliyosajiliwa kwa jina la Bupe Millinga yenye namba ya utambulisho ya mlipakodi (TIN) 135-563-382.

Ilidaiwa katika mashine hiyo kulikuwa na taarifa za mauzo ya Sh. bilioni 17.8, hivyo walikwepa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. bilioni 5.3.

Wakili huyo alidai katika shtaka la pili kwamba washtakiwa hao kwa pamoja walikwepa kulipa VAT Sh. bilioni 3.3 kwa kutumia mashine hiyo.

Katika shtaka la tatu na la nne, Medalakini alidai katika tarehe hizo washtakiwa walitumia mashine ya EFD kukwepa VAT ya Sh. bilioni 8.6.

Inadaiwa kati ya Januari na Juni 29, 2022, maeneo ya Kariakoo jijini Dar es Salaam, washtakiwa walitumia mashine isiyo sahihi ya Milinga kuonyesha ina mauzo ya zaidi ya Sh. bilioni 17.8 kwa lengo la kumdanganya Kamishna wa Mkuu wa TRA na kukwepa kodi ya Sh. bilioni 3.3.

Pia alidai washtakiwa kwa pamoja waliisababishia TRA hasara ya Sh. 8,691,535,718.50 (Sh. bilioni 8.69). Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo uliomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Medalakini alidai washtakiwa wanapaswa kuomba dhamana Mahakama Kuu kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kutoa dhamana kwa kuwa kiasi cha fedha kimezidi Sh. milioni 300.

Hakimu Tarimo aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 21 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wote walirudishwa rumande.

# TCU yafungua dirisha udahili wa vyuo vikuu

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imetangaza kufungua dirisha la maombi ya udahili kwa waombaji wa Shahada ya Kwanza kwa siku 29 kuanzia jana.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alitangaza kufunguliwa kwa dirisha hilo jana jijini Dar es Salaam ikiwa ni siku chache baada ya kutangazwa kwa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka huu.

Alisema TCU inahimiza waombaji wote kuendelea kupata taarifa sahihi kupitia tovuti yao na kuhudhuria maonyesho ya 17 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yatakayofanyika kwa siku sita kuanzia Julai 18, mwaka huu, viwanja vya Mnazi Mmoja ili kuonana ana kwa ana na vyuo vikuu.

"Kundi la waombaji wa udahili kwa mwaka wa masomo 2022/23, maombi yanahusu makundi matatu, wenye sifa stahiki za kidato cha sita, wenye sifa stahiki za stashahada au sifa linganifu na wenye sifa stahiki za cheti cha awali cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania," alisema.

Prof. Kihampa alisema maombi yanatakiwa kutumwa moja kwa moja kwenye vyuo ambavyo mwombaji amevichagua na kuchagua programu za masomo anazozipenda.

Pia aliwakumbusha waombaji kuzingatia masuala muhimu kama kusoma kwa makini mwongozo wa udahili uliotolewa na TCU na kuelewa kabla ya kuanza kutuma maombi yoyote ya udahili.

"Pia wanapaswa kuingia katika tofauti za vyuo ili kujua taratibu za kutuma maombi; kuyatuma vyuoni kupitia mifumo ya kieletroniki iliyowekwa na vyuo, kuwasiliana na vyuo husika kupata taarifa za kina.

"Waombaji wenye vyeti vilivyotolewa na mabaraza ya mitihani ya nje ya nchi ni lazima wawasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kwa vyeti vya elimu ya sekondari au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NECTVET) kwa vyeti vya stashahada ili kupata ithibaki ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kutuma maombi ya udahili," alisema.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), Dk. Suleiman Jafo (kulia), akishiriki usafi kabla ya kuzindua kampeni ya Bahari Safi Jukumu Letu, katika ufukwe wa Bahari ya Hindi, eneo la Hoteli ya Ramada Resort by Wyndham, Mtaa wa Kilongawima, Kata ya Kunduchi, Dar es Salaam jana, inayotekelezwa na Taasisi ya Mazingira na Uwezeshaji ya TEEMO, kwa ufadhili wa hoteli hiyo na Hoteli ya Giraffe Beach. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe na Balozi wa Mazingira nchini, Winfrida Shonde. **PICHA: JOHN BADI**

# ACT Wazalendo yaibuka na hoja tano za wananchi

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeibuka na hoja tano za wananchi wanaolalamikia kupanda kwa gharama za maisha, ukosefu wa ajira na miundombinu kuwa mibovu.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, alibainisha kuwa hoja hizo zimetokana na ziara ya viongozi wa chama hicho kwenye Jimbo la Mbagala mkoani Dar es Salaam.

Alizitaja hoja hizo zinajumuisha uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, suala la demokrasia, Tume Huru ya Uchaguzi na Katiba Mpya.

Shaibu alisema hoja hizo zimetolewa na wananchi baada ya chama hicho kufanya ziara ya siku nane katika kata 10 za jimbo hilo.

Alisema Sekretarieti ya Chama Taifa ilifanya ziara hiyo, ikiwa na malengo mawili; kuhakiki hali ya chama katika ngazi ya kata ya kuhamasisha usajili wa wanachama katika mfumo wa ACT Kiganjani na kusikiliza matatizo yao.

Pia kuwatembelea wananchi kwenye maeneo yao ya kazi, makazi na burudani kwa lengo la kusikiliza maoni, matatizo na ushauri wao kuhusu mwelekeo wa nchi kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kuhusu hoja ya kupanda kwa gharama za maisha na hali ngumu ya kiuchumi, Shaibu alisema wananchi walisema bidhaa muhimu za chakula, mafuta ya magari, bidhaa za ujenzi, nauli za daladala na mabasi ya mikoani zimepanda.

"ACT- Wazalendo tunarejea ushauri wetu uliotolewa na Msemaji wa Sekta ya Nishati, Isihaka Mchinjita, kuishauri serikali kuondosha Sh. 500 kwa kila lita zinazokusanywa kama tozo ambapo itahakikisha serikali inaweka ruzuku ya Sh. bilioni 152.5 kila mwezi badala ya Sh. bilioni 100 za sasa.

"Tunasisitiza umuhimu wa serikali kuingilia kati kwa kuyawezesha mashirika ya TIPER na TPDC (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania) kuagiza mafuta ili kuhakikisha unafuu zaidi unapatikana," alisema.

Shaibu alisema jambo la pili ambalo wananchi waliliibua ni uhaba wa ajira na matatizo ya wamachinga, bodaboda na wafanyabiashara kwenye masoko.

"Kwenye kata zote tulizopita, wananchi wanalia kuhusu matatizo ya ajira. Vijana wasomi wanaendelea kumiminika mitaani huku uchumi ukiwa hauzalishi fursa za kutosha, waliojiajiri kwenye sekta za bodaboda, machinga na wafanyabiashara masokoni, sekta ambazo zimeajiri vijana wengi, wametueleza kuwa serikali haijaweka mazingira rafiki kwao kufanya shughuli zao," alisema.

Shaibu alisema ACT-Wazalendo inaishauri serikali kufikiria upya mpango wake wa kuwapanga machinga ambao utazingatia maslahi yao mapana.

Kuhusu miundombinu, Katibu Mkuu huyo alisema wananchi wamelalamika huduma duni za barabara, afya na elimu zisizoendana na mahitaji halisi kutokana na wingi wa watu.

Alisema chama hicho kinaitaka serikali itekeleze pendekezo la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kumwajibisha mkandarasi kumaliza mradi wa mabasi yaendayo haraka kwa wakati na kulipa fidia.

"Serikali pia itenge fedha kujenga na kukarabati barabara za mitaa ya Mbagala ambazo zipo kwenye hali mbaya.

"Suala la demokrasia, Tume Huru ya Uchaguzi na Katiba Mpya, wameridhishwa na msimamo wa ACT-Wazalendo katika kupigania Tume Huru ya Uchaguzi na kiporo cha Katiba Mpya, wamesisitiza kimaliziwe kwa sababu Katiba Mpya ni takwa la Watanzania," alisema.

Kuhusu uwajibikaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Shaibu alisema maeneo mengi waliyotembelea, wananchi wamelalamikia kuwa duni.

"Kwenye mitaa mingi licha ya serikali kukusanya michango kwa ajili ya usafi, kampuni zinazopewa zabuni haziwajibiki kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Serikali za Mitaa zinalalamikiwa kuuza maeneo ya wazi, kutosoma mapato na matumizi na ufujaji wa michango ya ulinzi shirikishi," alisema.

Kutokana na hilo kiongozi huyo, Shaibu alisema ACT Wazalendo inaitaka serikali iache kuwakingia kifua viongozi wanapotaka kuwajibishwa kwa umma.

Shaibu alisema kutokana na uzoefu wa ziara hiyo, ofisi yake itatoa mwongozo maalum kwa viongozi wake wa mikoa na majimbo kwa ajili ya kuzisemea kero za maeneo yao na watapimwa katika hilo.

"Chama kitazindua hivi karibuni kupitia Halmashauri Kuu ya Chama Taifa, Sera ya Chama ya Machinga. Kwenye sera hiyo, tutaweka bayana hatua ambazo serikali inapaswa kuzichukua kuhakikisha machinga wanafanya shughuli zao kwa uhuru," alisema.

Pia alisema chama kitaendelea kutekeleza wajibu wake wa kupigania Tume Huru ya Uchaguzi na Katiba Mpya kwa njia mbalimbali ikiwamo kufanya makongamano ya kitaifa.

"Kongamano la nne la Kitaifa la Tume Huru ya Uchaguzi kuelekea Katiba Mpya litafanyika mkoani Tanga Julai 23, mwaka huu ambapo tutatathmini na kutoa mwelekeo wa ajenda ya mabadiliko kwenye maeneo hayo," alisema.

# Waziri mkuu wa zamani wa Japan auawa akiwa mkutano wa kampeni

**TOKYO, Japan**

WAZIRI Mkuu wa zamani wa Japan, Shinzo Abe amefariki baada ya kupigwa risasi wakati anahutubia kwenye mkutano wa kampeni katika mji wa Nara nchini Japan.

Katika shambulizi hilo lilofanyika jana asubuhi, Abe alikimbizwa hospitalini lakini baadae ilitangazwa amefariki dunia.

Waziri mkuu wa Japan Fumio Kishida, alitoa taarifa kuhusu kushambuliwa kwa Abe mapema asubuhi.

Abe alikuwa anahutubia kwenye mkutano wa kampeni kwa niaba ya chama chake cha Liberal Democratic.

Waziri Mkuu huyo wa zamani aliyekuwa na umri wa miaka 67, alizimia baada ya kushambuliwa na alionekana akivuja damu, kabla ya kupelekwa haraka hospitali ambako alifariki.

Polisi walisema wamemkamata mwanamume mwenye umri wa miaka 41, wanayemshuku kuhusika na tukio hilo. Shirika la habari la Japan (NHK) limemnukuu mtuhumiwa huyo Tetsuya Yamagami, aliyewaambia polisi kwamba alidhamiria kumuua Waziri Mkuu wa zamani Shinzo Abe kwa sababu hakuridhika nae.

Waziri Mkuu Kishida, alilaani vikali shambulizi hilo dhidi ya Abe lililotokea katika mji wa Nara ulio magharibi mwa Japan huku watu wa nchi hiyo na viongozi wa dunia wakionyesha kushtushwa na mauaji hayo katika nchi ambayo ni nadra kuwepo vurugu za kisiasa na kuna sheria kali za kudhibiti matumizi ya bunduki.

Waziri Mkuu Kishida alisema kuuawa kwa Shinzo Abe, ni kitendo kisichoweza kusameheka.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani Annalena Baerbock, ameelezea kushtushwa kwake na shambulio dhidi ya waziri mkuu wa zamani wa Japan Shinzo Abe. Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema ameshtushwa na shambulio lililosababisha kifo cha Shinzo Abe.

Alisema mawazo yako pamoja na familia, raia wa Japan na marafiki wa karibu wa waziri mkuu huyo wa zamani na kwamba Ufaransa inasimama na watu wa Japan katika wakati huo mgumu.

Abe alikua waziri mkuu wa Japan kwa muda mrefu zaidi kutoka mwaka 2006 hadi mwaka 2020.

Kufikia wakati wa majira ya joto mnamo mwaka wa 2020, umaarufu wake ulisambaratika kutokana na jinsi alivyoushughulikia mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 na pia kutokana na msururu wa kashfa ikiwemo ya kukamatwa waziri wake wa zamani wa sheria.

Alijiuzulu mwaka huo huo kwa sababu ya ugonjwa, lakini aliendelea kuwa maarufu katika siasa.

Wakati wa uongozi wake moja ya malengo yake makuu yalikuwa kuboresha ulinzi wa nchi yake na katiba ili Japan iweze kushiriki katika shughuli za kijeshi za kimataifa.

Mtuhumiwa aliyekamatwa anadaiwa kumfyatulia risasi mbili Abe kutokea nyuma na alitumia bunduki iliyotengenezwa nyumbani.

**DW**


**KIBAIGWA AUCTION MART & CO.LTD**
**P.O.BOX 621,**
**BABATI-MANYARA**
Email: kiamacoltd@gmail.com
Mob: 0784 718272/0755 706817

KIBAIGWA AUCTION MART & CO.LTD
NGARENARO STREET - BAGARA
P.O. BOX 621,
BABATI – MANYARA
MOB:0784 718272/0755 706817
Email: kiamacoltd@gmail.com

BRANCHES KITETO & MBULU
Tribunal Court Broker
&
COURT BROKER - MANYARA

TIN No. 139-244-184
Auctioneer, Court Broker, Debt, Eviction, Demolish Collector, Process Server Commission, Warehouse Operator & Attachment& Sale.

**TANGAZO LA MNADA**
**(WAKALI WA MINADA)**

KIBAIGWA AUCTION MART & COMPANY LTD Dalali wa Mahakama kwa idhini tuliyopewa na HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO - MANYARA tutakuwa na Mnada wa Hadhara wa kuuza Magari mawili na Mtambo mmoja chakavu tarehe **13/07/2022** siku ya Jumatano muda ni saa 4:00 asubuhi na kuendelea. Wananchi wote mnakaribishwa kwenye mnada wa Hadhara katika yadi ya Halmashauri ya Wilaya Kiteto (Idara ya Ujenzi).

| Jina la Mwenye mali | Aina ya Mali | Mahali mali ilipo | Muda wa Mnada | Idadi ya mali |
|---|---|---|---|---|
| HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO | 1. SM 2520 ISUZU<br>2. T 742 ABJ NISANI<br>3. MTAMBO (KATAPILA) | KWENYE YADI YA IDARA YA UJENZI -KITETO | MUDA NI SAA 4;00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MAGARI MAWILI NA MTAMBO MMOJA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Magari mawili na Mtambo yatauzwa kama yalivyo na mnunuzi atawajibika kubadilisha hati ya usajili wa Magari hayo kwa gharama zake mwenyewe.
2. Mnunuzi atalipa 25% ya bei ya Mnada papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka, na kiasi cha 75% iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) na iwapo atashindwa kulipa Mnada utatangazwa upya na fedha za awali haitarudishwa.
3. Siku za ukaguzi wa Magari na Mtambo ni tarehe 12/07/2022 siku ya Jumanne kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kwa kuwaona Maafisa ugavi Simu Na. 0655 303454, 0754 456171 Ofisi ya Ugavi Kiteto.
4. Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kibaigwa Auction Mart & Co. Ltd kwa Na. 0755706817, 0784718272.
5. Wananchi wote mnakaribishwa kwenye mnada wa hadhara tarehe **13/07/2022**. Karibuni sana

Jeremiah M. Mtagwa
**DALALI**

KIBAIGWA AUCTION MART & COMPANY LTD
P.O.BOX 621
BABATI-MANYARA

116937802

# CCM: Msimchukulie poa Samia

Na Romana Mallya

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema mtu ambaye hatakiwi kufanyiwa masihara katika kulinda rasilimali za nchi ni Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo kuwaonya wale wanaomchukulia 'poa'.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka alisema hayo jana alipofanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP na kujionea vinavyofanya shughuli zake.

Shaka alifanya ziara hiyo kwa lengo la kujifunza, kuimarisha uhusiano na kufungua milango baina ya chama hicho na vyombo vya habari vya taasisi hiyo.

Katika mahojiano maalum yaliyofanywa na vyombo vya habari vya IPP, Shaka alisema watu wanapomwona Rais Samia wasifirikie kwamba ndivyo alivyo katika undani wake lakini ni mtu makini anayesimamia kwa nguvu zote rasilimali za nchi.

"Tumeshuhudia wote na hatua zimeendelea kuchukuliwa. Wakati mwingine si lazima uchukue hatua ukataka tena dunia nzima ijue. Ziko hatua zinazochukuliwa za kinidhamu. Unaweza kusema kwamba kwa nini hatumwoni anatoka na kusema nimemfukuza huyu na huyu. Hiyo siyo sifa, kuna ubinadamu na kuna nidhamu ya kimaadili.

"Kwa sababu ni maelekezo ya chama na kila jambo liko kwenye maandishi na hakuna jambo limetoka mbinguni, chama tumesema katika kipindi cha miaka mitano tutahakikisha tunasimamia heshima ya matumizi ya fedha za serikali, fedha za walipakodi ili zilete tija na maendeleo endelevu," alisema.

Shaka alisema hayo baada ya kuulizwa juu ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hususani matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo kinyume cha malengo yaliyowekwa. Alisema wajibu wa chama ni kuishauri serikali na kwamba hakuna mbaye atafanya ubadhirifu na kukwepa mkono wa sheria.

"Bahati nzuri Watanzania sasa ni waelewa mno. Leo hii nenda kajenge kituo cha afya Kakonko chini ya kiwango uone Watanzania watakavyopiga kelele. inawezekana CAG akachelewa kufika.

"Watanzania kabla CAG hajafika wao wenyewe wanatosha kuwa Ma-CAG. Kiwango cha uelewa kimekua hasa kwenye miradi ya maendeleo. Kwenye ziara wanatuambia, 'Katibu wa Itikadi umekuja lakini hiki ni kituo cha afya kweli?'" alisema.



Katibu wa NEC ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari katika studio za ITV jana alipofanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

### MACHINGA KURUDI

Kuhusu wafanyabiashara wadogo, maarufu kama machinga, Shaka alisema CCM imefanya tathmini ya kina kama ilivyofanya kwenye asilimia za mikopo kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

"Maeneo hayo mtambuka tumeyafanyia tathmini na wiki kama mbili tumepokea ripoti yake na yapo mambo ya kufanyia kazi. Kama chama tunafuatilia kwa karibu kwa sababu mwisho wa siku Chama Cha Mapinduzi ndiyo matajiri, serikali tumewapa duka watuuzie, wateja wetu ni wananchi lazima tuwe nao karibu, tujue bidhaa tunazowauzia zinauzika na wanaridhika.

"Tumefanya utafiti na tathmini ya kuona namna nzuri ya makundi haya likiwamo la machinga namna ya kurasimisha biashara zao. Tunashukuru bajeti ya mwaka huu wa fedha 2022/23, Rais Samia ametenga karibia Sh. bilioni 10, hivyo tathmini hii itatupa mwelekeo itumikeje," alisema.

Hata hivyo, alisema CCM itaishauri serikali namna nzuri inayopaswa kufanyika na maeneo ambayo watafanyia biashara. Alitoa mfano wa Dodoma ambako ujenzi unaendelea kwa kutumia fedha za UVIKO-19 na maeneo mengine pamoja na changamoto ikiwamo Dar es Salaam ambako mambo yanakwenda vizuri.

"Huwezi kukamilisha kwa asilimia 100 ndani ya kipindi kifupi. Utakwenda hatua kwa hatua lakini mwisho wa siku mtafikia malengo," alibainisha.

### AJIRA

Shaka alisema mradi wa kimkakati wa gesi wa Lindi ndio mkubwa ndani ya mwaka mmoja wa Rais Samia ambao wanaamini utapunguza tatizo la ajira kwa vijana na rika zingine kwa asilimia kubwa.

Alisema waliahidi ajira milioni nane kwa kipindi cha miaka mitano na tathmini ya awali inaonyesha wanakwenda vizuri na wanaamini serikali ikiendelea hivyo kazi yao 2025 itakuwa nyepesi.

### HOJA KATIBA MPYA

Kuhusu hoja ya Katiba Mpya ambayo hivi sasa kumekuwa na vilio kila kona, Shaka alisema suala hilo linazungumzika na kwamba waliobeba hoja hiyo tangu mwanzo ni CCM, hivyo hilo si jambo geni.

"Tumeshauri serikali wote mtakuwa mashahidi. Rais Samia alipoingia madarakani alisema 'Nipeni muda'. Tumempa na tumeona mabadiliko makubwa yamefanyika. Kwanza ameimarisha mfumo wa demokrasia na alivyosema 'Ninataka kufungua nchi' wengi wakafikiria atakuja na kufuli na ufunguo aseme 'sasa nafungua nchi'.

"Amefungua fursa za kiuchumi, amefungua uhusiano wa kikanda na kimataifa. Tulipofikia tukasema chama hiki ni cha watu na kinachosikiliza na kimebeba ajenda ya taifa, tukasema sasa ni muda muafaka wa kuishauri serikali kuangalia namna bora ya kufufua mchakato wa Katiba, tutakwendaje ndiyo maana tunashauri serikali kaeni mje na kwetu kwa sababu katiba si ya wanasiasa ni ya wananchi.

"Tukisema tulibebe wanasiasa hatutawatendea haki Watanzania. Lazima kuwe na mfumo shirikishi, wanaweza kuuliza washirikishwe mara ngapi? Hata tukianzia kwenye Katiba Inayopendekezwa lazima washirikishwe lazima turudi kwa wananchi wajue uamuzi utakaochukuliwa kwa mustakabali wa kizazi cha sasa na kijacho," alibainisha.

"Kwa CCM suala la Katiba Mpya si jambo jipya ni mwendelezo tu wa namna ya kusikia mwelekeo na kusikiliza ya walio wengi na wataendelea kufanya hivyo. Hata la tume wamepewa nafasi na baadhi ya vyama wamepewa nafasi kuwasilisha mawazo," alisema.

### UHURU VYOMBO VYA HABARI

Kuhusu uhuru wa vyombo vya habari, kiongozi huyo alisema kuna mafanikio makubwa tofauti na kipindi kilichopita. Alisema kwa sasa watu kupitia tasnia ya habari wanakosoa na kutoa yao ya moyoni na serikali inawasikiliza kama Rais alivyowahi kusema vikosoe kwa staha kwa kutanguliza utaifa, uzalendo na kushauri inapobidi.

"Utakapokosoa kwa jazba au kutengeneza propaganda za kuchochea mambo ambayo hayana mustakabali kwa taifa, tukumbuke hapotezi mtu mmoja bali tutapoteza wengi pengine na kizazi kinachokuja. Tushukuru (wanahabari) mna amani mnafanya kazi zenu vizuri. Hata vyombo vilivyokuwa vimefungiwa vimefunguliwa na ambaye hajaanza kufanya kazi ni yeye mwenyewe.

"TV mtandaoni zilikuwa changamoto. Ile ni sehemu ya kijana kujiari, sasa unapomwambia kujisajili tu akalipe Sh. 500,000 mpaka 1,000,000 ilikuwa vigumu. Rais Samia amepunguza tozo kwa sasa ni Sh. 50,000 mpaka 200,000. Serikali zote (ya Muungano na ya Zanzibar) zinaendeleza azma yake kulinda na kuimarisha utawala bora, utawala wa sheria na uhuru wa vyombo vya habari," alisema.

### ANDIKO LA RAIS

Kiongozi huyo alimshukuru Rais kwa andiko lake aliloliandika kwa vyombo vya habari hivi karibuni na kueleza kuwa lina nia njema juu ya mustakabali wa nchi. Alisema walikotoka ni kuzuri, walipo ni kuzuri zaidi na wanakokwenda matarajio ni makubwa zaidi.

"Tukijitathmini namna tulivyokuwa tunafanya siasa miaka mitano iliyopita, siasa zimebadilika ndani ya mwaka mmoja. Leo tunazungumzia maridhiano ya vyama vya siasa, nani alikuwa anazungumzia miaka mitano iliyopita? Tunazungumzia vyama vya siasa kujifungia kutathmini mwelekeo wao," alisema.

Shaka alisema andiko la Rais, limewarudisha kwenye uzalendo na utaifa na kuwakumbusha wajibu wao kama Watanzania kwamba vyama vingi vya siasa siyo chuki, uadui wala uhasama, bali vitumike kama kichocheo cha maendeleo.

"Kama tutaishi kwenye maono ya Rais Samia, nchi hii itapiga hatua kubwa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Nimeona dhamira ya dhati ya Rais Samia kupitia andiko hili. Hata shughuli zetu za siasa huko mbele, ninaamini kabisa chini ya uongozi wa Rais Samia yawezekana Tanzania tukafanya uchaguzi wa kihistoria 2024 na 2025 kwa sababu ya dhamira na utayari wake.

"Wengine wanasema hahofii chama chake, hawezi kuhofia chama chake ni chama kikubwa, ni chama ambacho kinaaminika, kimebeba matumaini na hatima ya Watanzania. Kimejipambanua ndiyo maana tunasema ni chama kiongozi.

"Andiko la Rais litusukume na liwe funzo kwetu wanasiasa na hata ninyi wana tasnia ya habari na nyingine. Tutumie kama kielelezo na sehemu ya kutukumbusha tulikotoka, tulipo na tunakokwenda," alisema.

# Mkemia atoa zawadi waliong'ara sayansi

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imetoa zawadi kwa wanafunzi 36 wa kidato cha nne (2021) na sita (2022) waliofanya vizuri katika masomo ya sayansi.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelix Mafumiko, akitoa zawadi hizo jana kwa wanafunzi hao na walimu sita wa masomo ya sayansi, alisema ni mpango wa GCLA katika kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo hayo.

"Serikali inafanya jitihada kuhakikisha watoto wanapata elimu katika ngazi zote na inatoa fursa kwa wanafunzi wa sayansi kwa kutenga shule maalum, kujenga maabara na vifaa vya kujifunzia, nasi kwa nafasi yetu tumekuwa tukitoa zawadi kwa wanafunzi na walimu," alisema Dk. Mafumiko.

Mwenyekiti wa Bodi ya GCLA, Prof. Ester Rugwisha, alisema sayansi ni muhimu katika maisha ya binadamu na majukumu ya ofisi ya Mkemia yamekuwa katika masomo hayo kama vile uchunguzi wa sampuli mbalimbali.

"Sayansi inatengeneza kemia, fizikia na baiolojia, itatengeneza wataalamu mbalimbali wa sayansi kama wafamasia, wahandisi, madaktari na makundi mengine.

Prof. Rugwisha aliwapongeza wanafunzi kwa kuibuka videdea pamoja na walimu kufanya kazi kubwa ya kufundisha kwa bidii.

Alisema utoaji zawadi utafanya wanafunzi kufanya jitihada na pia walimu kufundisha kwa bidii ili kuwa na nchi ya viwanda kutokana na kuwa na wanasayansi wengi.

Alisema ili kuongeza hamasa zaidi, zawadi za kidato cha nne zimeongezeka kutoka Sh. 550,000 hadi Sh. 700,000; nafasi ya pili kutoka Sh. 500,000 hadi Sh. 650,000 na nafasi ya tatu kutoka Sh. 450,000 hadi Sh. 600,000.

Kwa kidato cha sita, zawadi zimeongezwa kutoka Sh. 700,000 hadi Sh. 800,000, nafasi ya pili kutoka Sh. 650,000 hadi Sh. 750,000 na nafasi ya tatu kutoka Sh. 600,000 hadi Sh. 700,000. Alisema kwa upande wa walimu, kila mmoja atapewa Sh. 700,000.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa elimu bure, hakuna sababu ya mzazi kujitetea kushindwa kumsomesha mtoto wake," alisisitiza.

Mwalimu wa kujitolea wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kichanga Chui iliyoko mkoani Kigoma, ni miongoni mwa walimu sita waliopewa zawadi.

Mwalimu huyo ambaye alipewa zawadi baada ya kuwa kinara katika somo la Fizikia, alisema licha ya kufanya kazi katika mazingra magumu, amekuwa akijitoa kuhakikisha wanafunzi wake wanafanya vizuri.

Mwanafunzi Yohana Katani wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Mzumbe, aliishukuru mamlaka hiyo kwa kuwatia moyo kuendelea kusoma sayansi.

"Tunawashukuru wote wanaohamasisha na kuwetuwezesha ili kufikia ndoto zetu, vitu vikubwa vinavyochochea uzalendo kwa mtoto ni pale anaposaidiwa kupata suluhu ya matatizo," alisema,.

Tangu kuanza kwa utoaji wa zawadi hiyo mwaka 2007, jumla ya wanafunzi 312 na walimu 36 wametunukiwa.

# TANESCO yatangazia kiama makandarasi janja

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida limewaonya makandarasi watakaofanya kazi bila kuzingatia taratibu na miongozo iliyowekwa na kwamba watakaobanika watafutiwa leseni.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Singida, Florence Mwakasege, alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mambo mbalimbali likiwamo la huduma mpya ya NIKONEKT ambayo wateja watakuwa wakiomba kuunganishiwa umeme kwa njia ya simu au kompyuta.

Alisema kumezuka tabia baadhi ya makandarasi waliosajiliwa kwa kazi za kuweka mfumo wa umeme kwenye nyumba za wateja na TANESCO inapokaga kuangalia kitu gani kinatakiwa, lakini wanakuta hakuna utandazaji wa nyaya za umeme uliofanyika katika nyumba husika.

"Nawakumbusha makandarasi utendaji kazi, tutachukua hatua mkandarasi yeyote ambaye atakwenda kinyume cha utaratibu wa kazi na miongozo inavyotakiwa.

Tutachukua hatua mpaka kuwafuta kufanya kazi za TANESCO na tutawajulisha EWURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji) leseni itafutwa," alisema.

Kuhusu huduma ya NIKONEKT, Mwakasege alisema imerahisisha na kupunguza gharama na janjajanja kwa wananchi kwa kuwa awali ilikuwa lazima mwananchi afike ofisi za TANESCO kwa ajili ya kuomba kuunganishiwa umeme.

"Huduma ya NIKONEKT mwananchi anakuwa nyumbani kwake anatuma maombi kupitia simu au kompyuta na Tanesco inamfikishia huduma ndani ya siku nne na ikichelewa haizidi siku saba, mwananchi anakuwa amepata huduma kufanya maombi na kulipia gharama," alisema.

Alisema huduma hii tangu imeanza Mei 30, mwaka huu, katika Mkoa wa Singida, hadi juzi takribani siku 37 TANESCO imepokea maombi 2,500 ya wahitaji wa umeme na kwa siku wanaolipia ni takribani 70.

Kwa mujibu wa meneja, kati ya wateja walioomba huduma kupitia mfumo wa NIKONEKT waliolipia ni 930 na wateja 606 wameshaunganishiwa umeme na kazi inaendelea kufanyika.

Mwakasege alisema Mkoa wa Singida umejaliwa kuwa na kiwango kikubwa cha umeme lakini watumiaji bado ni wachache ambapo kiwango kinachotumika ni Megawati 15 wakati kiwango kilichopo ni megawati 100.

Nitoe wito kwa wawekezaji kuja kuwekeza katika Mkoa wa Singida tuna umeme wa kutosha kuwafikia na kuwahudumia kadri wanavyohitaji. Umeme upo mwingi sana msitumie umeme kwa kuwasha taa bali hata kwenye saluni na viwanda vidogo," alisema.

Katika hatua nyingine, meneja huyo aliwaonya watu wanaosafisha mashamba wakati wa misimu ya kilimo kuwa waangalifu wasiunguze miundombinu ya umeme.

"Mwananchi ambaye tutamkamata amechoma moto eneo lake akaunguza miundombinu atachukuliwa hatua za kisheria na vyombo vya usalama vina taarifa na vimejipanga," alisema.

Mwakasege pia aliwaomba wananchi kuwa walinzi wa miundombinu ya Tanesco kwani miundombinu siyo mali ya Tanesco ni ya Serikali ambayo inajumuisha wananchi.




Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Mcha Hassan Mcha (kulia), akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa mamlaka hiyo, alipotembelea maonyesho hayo, mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makusanyo msajili hazina yazidi kupaa

**Na Mwandishi Maalumu**

OFISI ya Msajili wa Hazina imekusanya mapato yasiyo ya kodi Sh. bilioni 852.98 sawa na asilimia 109.50 ya lengo katika mwaka wa fedha wa 2021/22 ulioishia Juni 30, mwaka huu.

Awali, ofisi hiyo inayosimamia taasisi, mashirika ya umma, wakala za serikali na kampuni ambazo serikali ina hisa, ilipangiwa kukusanya Sh. bilioni 779.03.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Msajili wa Hazina iliyotiwa saini na Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, fedha zilizokusanywa ni ongezeko la Sh bilioni 214.11 kutoka Sh. bilioni 638.87 zilizokusanywa mwaka 2020/21 ikiwa ni sawa na ukuaji wa asilimia 33.50.

Benedicto katika taarifa hiyo alisema ongezeko hilo ni matokeo ya kuimarika kwa shughuli mbalimbali za uchumi chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ambao umechochea uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini.

Alisema sababu nyingine ni uhusiano mzuri kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na taasisi zote inazozisimamia; kudhibiti matumizi pamoja na kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi na mashirika ya umma.

Ofisi ya Msajili wa Hazina inayosimamia taasisi, mashirika ya umma, wakala za serikali na kampuni ambazo serikali ina hisa pamoja na kupongeza kwa upatikanaji wa fedha hizo zinazokwenda kufanyakazi kuleta maendeleo ya nchi kwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hatimaye ukuaji wa uchumi wa Taifa, wameendelea kukumbusha uzingativu wa dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

Aidha, imetaka kuzingatiwa kwa dhima kuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2022/23 ambayo ni "Kuongeza Kasi ya Kufufua Uchumi na Kuimarisha Sekta za Uzalishaji kwa ajili ya Kuboresha Maisha".

"Ofisi ina matumaini makubwa kwa taasisi, mashirika ya umma, wakala za serikali na kampuni ambazo serikali ina hisa katika kuboresha utoaji huduma, kukuza biashara na kuhakikisha kuna tija kwenye utekelezaji wa shughuli zao zote," ilisema sehemu ya taarifa hiyo. Alisema ofisi yake itaendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu uwekezaji wa serikali kwenye taasisi, mashirika ya umma na kampuni ambazo serikali ina hisa pamoja na kuishauri serikali kuhusu uwekezaji kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za serikali. Alitaka menejimenti zote kutambua kuwa "Uwekezaji ni Msingi wa Maendeleo Endelevu" na kuendelea kuchagiza maendeleo kwa fikra hizo. Ofisi ya Msajili wa Hazina ndiyo msimamizi mkuu wa uwekezaji wa Serikali kwa niaba ya Rais na imekuwa pia na jukumu la kusimamia Ubinafsishaji wa Mali za Umma, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Mashirika ya Umma, Ukusanyaji wa Madeni ya Serikali yaliyorithiwa kutoka kwa lililokuwa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (CHC), na Urekebishaji na Ufilisi wa Mali zisizozalisha faida katika kampuni au mashirika yaliyobinafsishwa.

Kwa sasa, Ofisi ya Msajili wa Hazina inasimamia taasisi na mashirika ya umma 287, ikijumuisha kampuni na taasisi 40 zinazomilikiwa na serikali kwa hisa chache na taasisi 10 za nje ya nchi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera TFF, wadhamini kwa kuchagiza ushindani

**MSIMU** wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/2022 ulimalizika Juni 29, mwaka huu kwa timu zote 16 zilizokuwa zinachuana kushuka dimbani kumalizia ngwe yake kwa mujibu wa kanuni, kwa sababu tayari mshindi bingwa aliyekuwa anatafutwa alishajulikana.

Bingwa huyo si mwingine, ni Yanga ya jijini Dar es Salaam ambayo imemaliza msimu bila ya kufungwa mechi hata moja.

Kama ilivyo kanuni, msimu mpya hufunguliwa na mechi ya Ngao ya Jamii, basi pazia la msimu husika hukamilishwa na hafla ya kukabidhi tuzo kwa wachezaji, waamuzi, wadau na viongozi mbalimbali waliofanya vizuri.

Sherehe hizo zilifanyika jijini juzi usiku na kuhitimisha rasmi safari ya msimu uliopita kwa kukabidhi tuzo kwa waliofanya vizuri lakini pia walioutendea haki mchezo wa soka nao walipata Tuzo za Heshima kutoka kwa Rais wa TFF, Wallace Karia.

Utolewaji wa tuzo hizo unaweza kuonekana kama hauna maana kwa baadhi ya wadau kwa sababu majibu yake hujulikana wakati tayari wameshamaliza msimu lakini ni kweli tuzo hizo zinachangia katika kukuza maendeleo ya mchezo huo unaopendwa zaidi duniani.

Wachezaji wamekuwa wakipambana kufanya vizuri kwa sababu wanafahamu mwisho wa msimu watapata tuzo na zawadi kutoka kwa wadhamini mbalimbali waliopo kwenye mashindano wanayoshiriki.

Tuzo zimekuwa ni moja ya kichocheo muhimu katika kuongeza na kukuza viwango vya wachezaji kwa sababu wanaamini mbali na kujiongezea soko kuelekea dirisha la usajili, lakini heshima wanayopata baada ya kutangazwa washindi imesaidia kuwaimarisha kwa ajili ya msimu unaofuata.

Wakati msimu unaanza, wachezaji kila mmoja huzungumza amejipanga kuisaidia timu yake kufanya vizuri huku wengine wakiweka wazi wanahitaji kumaliza msimu kwa kutwaa ubingwa au kwenye nafasi nne za juu, lakini kadri mechi zinavyozidi kuchezwa, fikra na malengo hubadilika na hapo ndio ushindani huonekana.

Kwa mfano katika tuzo ya Mfungaji Bora iliyochukuliwa na mshambuliaji wa Geita Gold FC ya mkoani Geita, George Mpole aliyepachika wavuni mabao 17, awali ilionekana kama itabebwa na staa wa Yanga, Fiston Mayele, mafanikio ya mshindi huyo wa tuzo, kuliwafanya wachezaji hao wawili kuongeza juhudi kila waliposhuka dimbani na ushindani huo ulichangia kuiongezea thamani Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ni ukweli usiofichika, idadi ya mashabiki waliokuwa wanaifuatilia Geita Gold ikicheza, iliongezeka kwa sababu tu walikuwa na mchezaji anayeshindana na nyota kutoka kwa waliokuwa vinara wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Lakini kubwa lililoifanya ligi iliyomalizika kuwa tamu ni zawadi ya fedha zilizotangazwa kutolewa na Kampuni ya Azam Media, ambayo imepewa haki za matangazo ya televisheni. Msimu huu timu zote zimevuna fedha, lakini kiasi kikitofautiana kulingana na nafasi ambayo timu yao imemaliza kwenye msimamo wa ligi. Licha ya mafanikio yanayoonekana kupitia tuzo hizo, TFF kupitia Kamati ya Tuzo, msisahau kuyafanyia kazi maoni mbalimbali yanayotolewa na wadau ambao kwa kiasi kikubwa yanalenga kuzifanya tuzo hizo kuwa bora na kufikia kule walipokusudia.

Inaweza kuwa ni maboresho kama ambavyo tumeshuhudia kwa mara ya kwanza tuzo mpya wachezaji waliofanya vizuri katika Ligi ya Championship na First League. Tunaamini mabadiliko hayo yamefanyika kwa maslahi na afya ya soka na si vinginevyo.

Tunahitaji kuona msimu ujao wachezaji, timu na maofisa wote wanaoshiriki katika ligi zote zinazosimamiwa na TFF wanaendelea kujipanga kufanya vizuri kwa sababu wanaamini mwisho wa msimu watakabidhiwa tuzo ambazo baadhi yake zinafuatana na zawadi ya fedha.


Tunaamini ushindani huu wa kuwania tuzo za TFF, si tu unasaidia kukuza kiwango cha soka cha hapa nchini, lakini unakuwa ni sehemu ya kuziimarisha timu zetu zinazokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Hongera kwa washindi wote waliopata tuzo za msimu wa 2021/2022.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kanuni hii ya 'play off' mbili Bara ibadilishwe

**KESHO** ndiyo mwisho kwa wadau wa mpira wa miguu nchini kutuma mapendekezo ya maboresho ya kanuni za msimu ujao wa mashindano yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF).

TFF ilishatangaza huko nyuma kwa wadau wote na wapenzi wa soka kutuma mapendekezo, kitu chochote ambacho anataka kiongezeke katika kanuni za msimu ujao ili kuiboresha ligi hiyo.

Kuna kanuni kandamizi ambayo nataka iondolewe, lakini pia kuna wanaotaka kanuni hizo hizo ziwepo, lakini zifanyiwe marekebisho.

Kinachofanyika ni kuchukuliwa maoni hayo na kuchakatwa, kabla ya kutolewa rasmi na kuanza kutumika kwa msimu husika.

Ili kusiwe na malalamiko yoyote, TFF imetoa anwani yake ikitaka maoni au mapendekezo yatumwe kupitia email yao, maoni@tff.or.tz.

Kwa wadau wa soka bado hawajachelewa, wanatakiwa watume ili baadaye kusiwe na malalamiko kwa TFF wakati watakapozitumia.

Tumekuwa tukiona viongozi, waandishi wa habari na wachambuzi wa masuala ya michezo wakilalamikia baadhi ya maamuzi yanayotolewa na Kamati ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ligi kwa madai kuwa hayakutenda haki, au yamepitwa na wakati. Lakini kwenye nyakati kama hizi huwa hatuwasikii wakipeleka maoni mapya, au kuhitaji marekebisho ya kanuni zilizopita.

Hiki ndiyo kipindi ambacho husikii wachambuzi au mashabiki wa soka wakihamasishana kupeleka maoni, lakini ngoja siku maamuzi ya adhabu yatoke kwa mujibu na kanuni ambazo zimeletwa, kuchakatwa na kupitishwa na kamati husika, ndipo mapovu yanapoanza kuwatoka.

Uzuri ni kwamba maoni anapeleka mtu yoyote, shabiki, mpenzi, mwandishi, mchambuzi, mdau, kiongozi wa soka na yoyote yule anayeguswa na mchezo huo. Hayabagui.

Huwa nashangaa sana wanavyokurupuka na kulalamika mtu anayefungiwa kujihusisha na soka miaka mitano kuwa ni mingi na imepitwa na wakati.

Huu ni wakati sasa wa kupeleka maoni mfano kusiwe na kufungiwa maisha, bali kifungo kirefu kiwe miaka mitano na kifupi mwaka mmoja. Labda kufungiwa maisha iwe tuhuma za kupanga matokeo.

Zipo nyingi kama vile timu za nyumbani ziendelee kuchukua mapato, irekebishwe zigawane nusu kwa nusu, au wa nyumbani achukue asilimia nyingi kidogo, lakini mgeni naye apate.

Nilimsikia kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi akilalamika kuhusu kukatazwa kucheza wachezaji wote 12 wa kigeni waliosajiliwa kwenye Ligi Kuu, badala yake wanatakiwa kucheza nane kwa mechi moja.

Si yeye tu, mashabiki wengi wanaipinga kanuni hiyo, huu sasa ndiyo wakati wake wa kwenda kupeleka maoni kuwa irekebishwe, wachezaji wote wanatakiwa waanze iwe wa Kigeni au Kibongo bila ubaguzi. Wanataka mwenye uwezo aachwe acheze.

Kuna faini za timu kupitia milango isiyohusika. Wengi wanalalamika, wanasema ni ndogo sana na ndiyo maana timu hazijali, zinaendelea tu na tabia hiyo.

Kinachotakiwa sasa ni kupeleka maoni ya kutaka faini iongezwe, ili timu ikipigwa, basi isijifikirie tena kurudia kosa.

Leo mimi pendelezo langu ni mechi za mchujo ambazo kwa sasa zinaendelea. Hazitendi haki. Prisons ambayo imefungwa na Mtibwa Sugar, eti inakwenda kucheza 'play off' ya pili.

Haya ni matumizi mabaya ya rasilimali na muda. Pia kutozitendea haki timu za Championship.

Ikumbukwe JKT Tanzania ilishika nafasi ya tatu, ikaifunga Kitayosce iliyoshika nafasi ya nne, leo hii ikija kufungwa na Prisons na kukosa kurejea Ligi Kuu ni jambo linalokatisha tamaa.

Haiwezekani timu iliyofungwa kwenye Ligi Kuu iende kucheza na timu iliyoshinda Championship halafu aliyefanya vibaya kwenye Ligi Kuu anarejea tena kwa sababu kashinda mechi ya pili ya mchujo.

Kanuni hii haina mashiko, inabidi ibadilishwe kwa mustakabali wa soka la Tanzania. Tangu kanuni ya 'paly off' ianze imeonekana kuzinufaisha zaidi timu za Ligi Kuu zaidi kuliko za chini ambazo inabidi ndiyo ziandaliwe mazingira ya kutengenezewa kanuni ya kuwathamini zaidi.

Mawazo au maoni yangu ni kwamba kuanzia msimu ujao ni kwamba kila timu zicheze 'play off' moja zenyewe. Za Ligi Kuu zicheze yao na za Championship zicheze ya kwao na timu itakayoshinda inapanda na itakayofungwa inateremka moja kwa moja ili kurahisisha kazi na kuweka usawa pia.

Mfano kwenye ushindi wa jumla Mtibwa Sugar ilishinda, hivyo ilibidi ibaki Ligi Kuu na Prisons ishuke. Na Championship, JKT Tanzania ilitakiwa iwe tayari nayo imepanda Ligi Kuu.

Nadhani hapa tutakuwa tunatenda haki zaidi, hivyo ushauri wangu msimu ujao kanuni hii ibadilishwe kwa sababu inaleta ukakasi na ni kandamizi kwa timu za madaraja ya chini.

HABARI PICHANI

# ZIARA YA KATIBU WA NEC YA CCM ITIKADI NA UENEZI VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Mhandisi wa mitambo wa uchapishaji magazeti wa TGL, Christian Ngwapaula (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka. Kulia niMhariri wa Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago na Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga.



Mhariri wa Gazeti la Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago (kulia), akifafanua jambo kwa Katibu wa Halmashauri Kuu yaTaifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alipotembelea ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga.



Mkuu wa Chumba cha Habari cha ITV, Steven Chuwa (kulia), akifafanua jambo kwa Shaka Hamdu Shaka.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile (kushoto), akizungumza na Katibu wa NEC ya CCM Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka.




Shaka Hamdu Shaka (kushoto), akizungumza katika studio za East African Redio.
**PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

# Maofisa kortini madai ubadhirifu

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, imewapandisha kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Igunga watumishi wawili wa halmashauri hiyo, kwa tuhuma za ubadhirifu wa Sh. milioni nne.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Wilaya ya Nzega, Mazengo Joseph, aliwataja watumishi hao kuwa ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nanga, Moshi Akida na Mwalimu wa Shule ya Msingi Chipukizi, iliyoko Kata ya Igunga Mjini, Andrew Rutha.

Mbele ya Hakimu Mkazi Lydia Ilunda, Mwendesha Mashtaka huyo alidai kuwa Akida ambaye ni mshtakiwa wa kwanza, anakabiliwa na shtaka la ubadhirifu wa Sh. 7,574,000 pamoja na matumizi mabaya ya madaraka.

Kwa mujibu wa Mazengo, kati ya Agosti, 2018 na Novemba 2021, mshtakiwa huyo alipewa dhamana na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ya kukusanya mapato katika kata ya Nanga, akiwa ofisa mtendaji wa kata hiyo.

Pia alidai kuwa licha ya kukusanya fedha hizo, hakuzipelekwa benki na badala yake alizitumia jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Alidai kuwa Rutha anashtakiwa kwa ubadhirifu wa Sh. milioni moja na kwamba kwamba kati ya Oktoba 23 na 26, 2015, wakati wa uchaguzi mkuu, alitakiwa wa kujenga vibanda vua uchaguzi lakini hakufanya hivyo na kujipatia kiasi hicho cha fedha.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka hayo, wote wawili walikana kutenda makosa hayo.

Washtakiwa wote wako nje kwa dhamana ya maandishi ya Sh. 7,574,000 kwa upande wa Akida na Rutha amedhaminiwa kwa Sh. 550,000 hadi Julai 28, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa.




Mkuu wa Maduka na bidhaa za Intanet Tigo, Mkumbo Myonga (katikati), akionyesha simu na zawadi kutoka Samsung, kwa ajili ya wateja watakaofika katika mabanda ya Tigo, katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam kwenye uwanja wa Julius Nyerere, Barabara ya Kilwa, jana. Kulia ni Meneja Mauzo wa Samsung, Moses Mtweve na Meneja Mkazi Samsung, Manish Jangra. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima kicheko msamaha wa bil. 3/- mbegu za alizeti

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Kilimo imeleta neema kwa wakulima wa alizeti mkoa wa Singida baada ya kusamehe deni la Sh. bilioni tatu lililotokana na mkopo wa mbegu walizokopeshwa katika msimu wa kilimo wa 2021/22.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, alitangaza uamuzi huo wa serikali jana wakati wa kikao maalum cha majumuisho ya ziara zake alizozifanya hivi karibu katika wilaya za mkoa huo na kusikiliza kero za wananchi.

Dk. Mahenge alisema Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alitangaza kusamehe wakulima mkopo huo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye viwanja vya Nanenane mjini Tabora. Alisema uamuzi huo ulifikiwa baada ya kuelezwa kuhusu changamoto waliyopata wakulima katika mbegu walizopewa za ruzuku katika Mkoa wa Singida ambazo baadhi ya maeneo hazikufanya vizuri, hivyo kusababisha mavuno kushuka kulinganisha na misimu mingine iliyopita.

"Serikali imeamua kutoa ruzuku asilimia 100 kwa mbegu za alizeti zilizotolewa katika msimu wa kilimo wa 2021/22, hivyo wakulima hawapaswi kudaiwa. Serikali imeamua kusamehe," alisema.

Uamuzi huo wa serikali ni neema kwa wakulima kwa kuwa hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Mahenge, alipofanya ziara kwenye wilaya zote za mkoa wakulima walilalamika kuwa msimu huu wa kilimo mavuno ya alizeti yamekuwa duni kutokana na mvua kunyesha chini ya kiwango. Walisema hali hiyo inawapa wakati mgumu watawezaje kurejesha fedha kutokana na mbegu walizokopeshwa na serikali. Katika kilo mbili ya alizeti iliyokuwa inauzwa kwa bei ya Sh.7,000, mkulima alitakiwa kuchangia Sh.3,500.

Dk. Mahenge alisema katika msimu wa 2021/22 mkoa ulipewa mbegu tani 453.6 zenye thamani ya Sh. bilioni tatu ambazo walikopeshwa wakulina kwa makubaliano kuwa watazirejesha baada ya mavuno.

Alisema mbegu hizo ziliwezesha kulima ekari 653,382.8 za alizeti na matarajio ya mavuno yalikuwa kupata tani 513.382.

Hata hivyo, kutokana na mvua kunyesha chini ya kiwango, uzalishaji umeshuka na kuwa tani 272 tu hali ambayo imesababishwa na mvua kutoshenya kwa wingi lakini pia mbegu walizopewa hazistawi vizuri katika baadhi ya wilaya

Dk.Mahenge alisema katika mkoa wa Singida kuna viwanda 243 vikubwa, vya kati na vidogo vya kusindika mafuta lakini malighafi haitoshi ndiyo maana mwaka jana uliwekwa mkakati wa kuongeza uzalishaji kwa kuwa ardhi ipo ya kutosha.

# Waonywa anasa matumizi ya pesa za mafao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MENEJA wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Shinyanga, Julius Mataso, amewashauri wastaafu kuwekeza fedha zao za mafao kwenye miradi yenye tija ili ziwaingizie kipato na kuendesha maisha yao kama kawaida, badala ya kuzifanyia anasa.

Ametahadharisha kuwa baadhi ya wastaafu wanapokuwa wakipata mafao yao, huchanganyikiwa na kushindwa kuamua fedha hizo wazifanyie vitu gani vya maendeleo, hivyo kuishia kizitapanya ovyo na kubaki maskini.

Alitoa angalizo hilo juzi alipotoa elimu ya kifedha kwa wastaafu wa Manispaa ya Shinyanga, akisisitiza wawe na matumizi sahihi ya mafao yao.

Meneja huyo alisema mstaafu anapopata mafao yake, anapaswa kwanza kutuliza akili na kuomba ushauri wa kitaalamu fedha hizo azifanyie kitu gani kitakachoendelea kumwingizia mapato kuliko kukurupuka na kuzifanyia anasa.

"Benki yetu ya TCB ina fursa nyingi kwa ajili ya wastaafu, na ndiyo maana tumewaita hapa ili kuwapatia elimu ya kifedha na kuwaonyesha fursa ambazo tunazo na wazitumie kuneemeka na mafao yao kuliko kuishia kwenye anasa," alisema Mataso. Alitaja fursa ambazo benki hiyo wanazo kwa ajili ya wastaafu kuwa ni pamoja na akaunti ya muda maalum, ambayo watawekeza fedha zao na kupata riba ya asilimia 10 na kutolea mfano kuwa akiwekeza Sh. milioni 100, riba yake kwa mwaka atapata Sh. milioni 10.

Alitaja fursa nyingine kuwekeza fedha zao kwenye akaunti ya kivulini, ambayo ina bima pamoja na fao la kifo na kufafanua kuwa mstaafu akifiwa na mwenza wake au mtoto ambaye ni tegemezi, atapewa pole ya Sh. milioni mbili.

Aliwataka wastaafu hao kutumia fursa ya mikopo iliyoko katika benki hiyo, akitamba kuwa mteja wao akifariki dunia, mkopo huo unafutwa.

"Benki ya TCB tuna fursa pia ya mikopo kwa ajili ya wastaafu, na kabla ya kupewa mkopo atapatiwa kwanza ushauri wa kitaalumu wa kwenda kuwekeza kwenye miradi yenye tija na inaendana na umri wao ili asiende kuzitumia fedha hizo vibaya mwisho wa siku anapata presha na kupoteza maisha," alisema Mataso.

Wastaafu hao akiwamo David Madata, walipongeza kupatiwa elimu hiyo ya kifedha na matumizi sahihi ya mafao yao, na kubainisha kuwa akili zao sasa zimefunguka kwa kuziwekeza fedha hizo kwenye miradi yenye tija na siyo kuishia kuzifanyia starehe.



# Wigo kilimo cha umwagiliaji sasa kufikia hekta milioni 1.2

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TUME ya Taifa ya Umwagiliaji imejipanga ndani ya miaka mitatu hadi mwaka 2025 kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 694,070 hadi milioni 1.2.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Raymond Mndolwa, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mikakati ya kupaisha kilimo cha umwagiliaji nchini.

Mndolwa alisema ili kuhakikisha lengo hilo linafikiwa, serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya

umwagiliaji iliyoharibika, isiyofanya kazi na kujenga skimu mpya.

"Tunakwenda kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kujenga skimu na mabwawa mapya ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya shughuli za

kilimo cha umwagiliaji," alisema. Mndolwa alisema tume hiyo inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Dira ya Taifa ya Maendeleo Awamu ya Pili, Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) na Mpango wa Umwagiliaji wa mwaka 2018.

Mndolwa pia alisema Wizara ya Kilimo kupitia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeiwezesha tume hiyo kwa kuongeza bajeti jambo ambalo linazidi kutoa hamasa ya kufanya kazi kwa bidii ili kupaisha sekta hiyo. Aliishukuru serikali kwa uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Tume hiyo sambamba na kibali cha ajira ya wataalamu 344 ili kuongeza nguvu katika kilimo cha umwagiliaji.



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoa wa Dodoma, Pili Mbanga (kushoto), akikabidhi fomu ya kugombea ujumbe wa halmashauri kuu ya CCM mkoa kwa Lukanus Kayombo, katika ofisi za chama hicho, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkakati wawekwa kudhibiti sumukuvu

**Na Renatha Msungu,**
CHEMBA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesema serikali inajenga maghala 14 yanayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 14 kwenye maeneo mbalimbali nchini yanayokabiliwa na tatizo la sumukuvu.

Mavunde aliyasema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa ghala kwa ajili ya kudhibiti sumukuvu unaotekelezwa kupitia Mradi wa TANIPAC katika Kijiji cha Mrijo Chini wilayani hapa.

Alisema mradi wa ujenzi wa ghala hilo ni mahsusi katika kukabiliana na tatizo la sumukuvu ambayo imekuwa ni kikwazo kikubwa katika wilaya hiyo.

"Tunajenga miradi ya namna hii kwenye maeneo 14 ikiwamo Chemba kama mnavyoona. Tutajenga pia maabara ndogo ambayo itapima mazao yanayokuja kwenye ghala hili. Serikali imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha tunadhibiti sumukuvu," alisema.

Alibainisha kuwa wakulima watapewa elimu ya namna ya kutunza mazao yao ili tatizo hilo lisijirudie.

"Tunaamini mradi huu utakuwa na tija kwenu na itaondoa tatizo hili kwa kuwa sumukuvu ina athari kubwa ndiyo maana serikali imeamua kufanya mradi huu. Eneo hili lina ukanda wa wakulima wengi sana na miongoni mwa mikakati tuliyo nayo ni kuongeza thamani ya mazao yetu. Tunataka wakulima wauze unga na si mazao," alisema.

Alisema kila mmoja anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzie ikiwamo kutoa taarifa kwa wahusika pale atakapoona uharibifu unafanyika kwenye miundombinu ya ghala hilo.

Pia alisema serikali imetenga Sh.bilioni 43 kwa ajili ya Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA) kuzalisha mbegu bora zenye kumnufaisha mkulima na kuleta mapinduzi kwenye sekta ya Kilimo.

Mavunde alisema lengo lao ni kuona mbegu bora za mazao zinapatikana kwa wingi ili kuepusha usumbufu kwa wakulima kuzipata pindi wanapoanza msimu wa kilimo.

Naibu Waziri Mavunde pia alimwagiza Mratibu wa Mradi huo, Clepin Josephat, kuchimba kisima cha maji ili kupunguza tatizo la maji kwa wananchi wa eneo hilo.

"Hatuwezi kutegemea mvua pekee yake kukuza kilimo cha nchi yetu,tunaweka mifumo ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu ili kutoa nafasi kwa Wakala wa Mbegu kuzalisha mbegu kwa wakati," alisema Mavunde.

Naye Josephat aliahidi kuendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa maghala hayo kama ilivyopangwa.

# BAKWATA yahamasisha waumini kushiriki sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma, Bashiru Hussein, amewataka mashehe, maimamu na walimu kutumia nyumba za ibada kuhamasisha wananchi kushiriki sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

Hussein alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa huku akiwataka viongozi hao kuhakikisha wanashirikiana na serikali ili waumini wao washiriki kikamilifu kwenye zoezi hilo muhimu.

"Viongozi wa dini wana jukumu kubwa la kuhakikisha sensa ya watu na makazi inafanikisha ili serikali ifikie malengo yake ya kupanga miopango ya maendeleo kwa Watanzania," alisema.

"Sisi tukiwa ni waumini wa dini ya Kiislamu, suala la sensa ni jambo halali na si dhambi kushirki kwa kuwa lina faida kwa maendeleo ya Watanzania wote.

"Ikifanyika sensa hiyo serikali itatambua mahitaji ya watu wake na itaweza kuwahudumia kulingana na bajeti itakayowekwa kwa ajili ya maendeleo," alisema.

Ili kufanikisha azma hiyo, aliwataka viongozi hao wa dini kuwa mabalozi wa kuelimisha waumini wao ili kuondokana na taarifa potofu wanazopewa.

Pia aliwataka viongozi hao kukemea taarifa hizo ambazo zinazotaka kukwamisha zoezi hilo kwa kuwa ni muhimu watanzania kuhesabiwa.

Mwenyekiti huyo aliwataka waumini kushirikiana na serikali katika kutoa majibu sahihi ya takwimu ya idadi ya watu wanaoishi nao kwenye familia zao ili serikali kuwatambua.

Alisema ushirikiano huo ni pamoja na wale wenye watu ambao ni wenye ulemavu na wanaoishi na vikongwe,kutowaficha na badala yake wazitoe taarifa zao zilizo sahihi.





Mjumbe wa kamati ya sherehe za kijadi za mwaka, Asha Makame, akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu sherehe hizo zinazofanyika Julai 17 mwaka huu huko Makunduchi, mkoa wa Kusini Unguja. Kulia ni Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hassan Haji. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaweka kipaumbele uchunguzi afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA YA Afya ya Zanzibar imesema imeweka kipaumbele katika uchunguzi wa afya katika maradhi mbalimbali kwa wananchi na kuwapunguzia mzigo wa kufuata tiba hizo nje ya nchi.

Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana wakati akizindua kambi ya uchunguzi wa maradhi mbalimbali kwa ushirikiano na madaktari bingwa kutoka Kuwait, hafla iliyofanyika Fuoni Kibondeni.

Alisema maradhi mengi huwasumbua wananchi na kupata matatizo ya tiba kwa sababu ya kukosa uchunguzi katika hatua za awali.

Mazrui aliyataja baadhi ya maradhi ambayo yamekuwa changamoto kubwa kwa afya za wananchi kwa sababu ya kukosa huduma za uchunguzi katika ngazi za awali kuwa ni pamoja na kisukari, shinikizo la damu na saratani.

Alisema tayari Wizara ya Afya imeanzisha kitengo cha uchunguzi wa maradhi na utafiti hatua ambayo itasaidia kujua kiini cha maradhi na kuyapatia tiba kwa haraka.

"Wito wa Wizara ya Afya tunawataka wananchi wajitokeze mapema kuchunguza afya zao zaidi wanapobaini mabadiliko yasiyokuwa ya kawaida katika miili yao. Wafike kuchunguza afya zao haraka kwa sababu kitengo kinachotoa huduma hizo kipo," alisema. Naye kiongozi wa timu ya madaktari kutoka Kuwait, Dk. Abdulla Buhana, aliipongeza Wizara ya Afya kwa kuwaruhusu kutoa huduma za afya za uchunguzi wa maradhi mbalimbali kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisema wamebaini katika uchunguzi wa afya za wananchi wengi katika ukanda wa Afrika Mashariki wanakabiliwa na maradhi yasiyoambukiza yakiwamo kisukari, shinikizo la dasmu na saratani ambayo yasipopatiwa tiba ya awali, husababisha kifo.

Dk. Buhana alisema wamejipanga kutoa huduma za afya kwa wananchi kadri itakavyowezekana kwa kushirikiana na madaktari wazalendo.

"Timu ya madaktari bingwa kutoka Kuwait tupo Zanzibar kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa maradhi mbalimbali yanayowakabili wananchi pamoja na kutoa matibabu ikiwemo upasuaji," alisema.

Mkurugenzi wa Kinga na Elimu ya Afya, Dk. Said Nyanga, ameipongeza serikali ya Kuwait kwa ushirikiano na Zanzibar ambayo imejikita katika sekta mbalimbali huku afya ikiongoza.

"Ushirikiano wetu na serikali ya Kuwait katika sekta ya afya ni mkubwa na matarajio yetu ni kusaidia katika utaalamu zaidi wa huduma za afya kwa wananchi wetu," alisema.

# AAFP yapongeza Kiswahili kuwa kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Wakulima (AAFP) kimesema uamuzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kukitambua Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa ni fahari kwa Tanzania na Afrika.

Mwenyekiti wa AAFP, Said Soud Said, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kwamba maadam Kiswahili kinatumika na kusikika kinatosha kuingizwa katika mitaala ya elimu.

Soud alisema ikiwa Russia, China, Japan, Uturuki na Ujerumani zinatumia lugha zao asilia, Tanzania isishabikie lugha za kigeni.

Alisema katika maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani, ushiriki wa marais Samia Suluhu Hassan na Philippe Nyusi wa Msumbiji kuhutubia kwa Kiswahili ni kielelezo cha utajiri wa lugha hiyo.

"Tumesubiri sana sasa kiingizwe kwenye mitaala ya elimu, kuanzia shule za awali hadi elimu ya juu. AAFP tunawasifu watetezi wa Kiswahili na uamuzi wa UNESCO kukitambua Kiswahili ni ushindi, alisema Soud.

Mwenyekiti huyo alisifu matamshi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Kanali Abdulrahman Kinana, aliyesema kiswahili kimetumika kuwaunganisha Watanzania.

"Kiswahili kimelinda utamaduni, mila, desturi na ustaarabu wetu. Ni lugha iliyoharakisha kuleta uhuru, mapinduzi na ukombozi kusini mwa Afrika," alisisitiza.

Mwenyekiti huyo alisema ni vigumu kuzungumzia umoja, uzalendo, upendo na mshikamano na kukiweka kando Kiswahili.

"Tunawapa hongera waandishi wa vitabu vya fasihi andishi na simulizi. AAFP kinapongeza waandishi mahiri kina Shaaban Robert, Saadan Kandoro, Shafi Adam Shafi, Bwana MSA na Haji Gora," alisema.

Soud alisema pamoja na UNESCO, Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kukitambua Kiswahili kimataifa, aliwataka waandishi wa habari, watangazaji na wazungumzaji watumie Kiswahili sanifu na fasaha.

# Tamasha la kijadi kuboreshwa zaidi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Utamaduni wa Mkoa wa Kusini Unguja, Othman Muhammed Abdallah, amesema wanatarajia kuziboresha sherehe za kijadi za mwaka kogwa kuwa za kimataifa ili kupata watalii wengi katika sherehe hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sherehe hizo ambazo hufanyika Kijijini Makundichi kila mwaka, alisema kuwa sherehe hizo wanakusudia kiziboresha kwa kuwa na tamasha kubwa ambapo mataifa mbalimbali yataonyesha mila na jadi zao.

Alisema hatua hiyo itaongeza hamasa na ari ya kuendeleza mila na urithi huo ambao tokea umeanza ni zaidi ya miaka 200.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya sherehe hizo, Hassan Haji alisema kuwa kwa mwaka huu sherehe hizo zitafanyika Julai 17, mwaka huu. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, Nape Nauye.

Mwenyekiti huyo alisema sherehe hizo pia zitahudhuriwa na wageni mbalimbali kutoka nje ya Zanzibar wakiwamo machifu 30 kutoka makabila tofauti ya Tanzania Bara.

Pia alisema sherehe hizo zitatangulizwa na mila za kijadi za watu wa Makundichi zikiwamo matambiko ambayo wamerithi kutoka kwa wazazi wao wa kijiji hicho.

Hata hivyo aliwataka wale ambao hutumia mwanya wa kufanya mambo maovu katika sherehe hizo, kujihadhari na kutojihusisha na mambo hayo.

"Wapo ambao wanazitumia kinyume na utaratibu sherehe hizi kwa kufanya mambo maovu vikiwamo vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Tunalaani vikali vitendo hivyo," alisema.



**LODY**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 9, 2022



# WATADUMU KWELI?

WASANII nyota wa muziki wa Bongo Fleva, Nandy na Billnas, wapo katika matayarisho ya mwisho ya ndoa yao.

Hata hivyo, kumekuwa na usiri kuhusu tarehe ya kufungwa kwa ndoa hiyo, kwani baadhi ya watu wanadai harusi yao itakuwa mwezi huu.

Nandy licha ya kupinga kwamba hawaishi pamoja, lakini anasema wamewekeana utaratibu wa kila mmoja kwenda kulala kwa mwenzake pale inapobidi.

Akizungumzia harusi hiyo, Nandy amesema haitakuwa ya kitoto, kwani itawachukua kama wiki mbili hivi kusherehekea pamoja na kupewa zawadi mbalimbali kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki.

Juzi mwimbaji huyo, amemuandikia Billnas ujumbe mzito, kuelekea siku muhimu ya ndoa yao.

"Nikiangalia kumbukumbu zetu nalia tu, Aaaaa bwana mie nimekubali tunapendana huu mwezi safari yetu inahitimishwa na Mungu, na ikawe kheri nakupenda mwenzio" ameandika Nandy.

Baadhi ya wachambuzi katika masuala ya burudani, wametoa maoni yao na kusema ndoa nyingi za mastaa zinakuwa na mbwembwe nyingi, lakini hazichelewi kwisha katika muda mfupi.

"Tumeshuhudia mastaa kadhaa wakiachana muda mfupi baada ya kufunga ndoa, tunaamini Billnas na Nandy hawataingia katika mfumo huu wa mbwembwe na kisha kutimuana," amesema Adam Juma.

Tayari maharusi hao, wamemtangaza msanii wa filamu Steve Nyerere, kuwa Mwenyekiti wa kamati ya ndoa yao.

BASI SAWA

## Dk Jerry aomba ‘urafiki na wewe’



MWIMBAJI wa Injili, Dk Jerry Maswaga, amerudi kivingine kwenye muziki huo na wimbo wake mpya ‘Naomba Urafiki Nawe’ akiwa ameshirikiana na mkongwe, Beatrice Mwaipaja

Akizungumza na BT, Dk Jerry, ameweka wazi kuwa mashabiki wa muziki huo wanaweza kupata wimbo huo mpya kwenye chaneli yake ya YouTube na mitandao mingine.

“Wimbo huu umebeba ujumbe mzito kwa wanadamu kutafuta urafiki na Mungu, naamini watu wengi watabarikiwa ila kikubwa naomba sapoti zaidi kutoka kwa mashabiki,” amesema Dk Jerry.

## Starshine humwambii kitu kwa Zuchu



Msanii wa Bongo Fleva, Starshine, ameimwagia sifa projekti ya Zuchu, 4.4.2 iliyotoka hivi karibuni ambayo  inatikisa chati mbalimbali za muziki.

Starshine ameliambia BT kuwa ndani ya 4.4.2 kuna ngoma mbili ambazo ni Fire na Jaro ambazo Zuchu amefanikiwa kuonyesha kiwango kikubwa cha mapenzi.

“Zuchu ameonyesha ufundi wa mapenzi kwenye Jaro na Fire, amenivutia naamini kila mwanaume kamili atakubaliana na mimi, amenivutia nimejikuta nampenda,” amesema Starshine anayetamba na wimbo Ananivuruga.



## LODY MUSIC KUMBE ALIPAGAWA NA HAWA

MWIMBAJI wa ngoma kali, Lody Music amemtaja Aslay, Marioo na Bright Music kama ni baadhi ya wasanii aliopenda kuangalia kazi zao kabla ya kuwa maarufu.

“Kabla ya kuingia kwenye mziki nilikuwa napenda kuangalia movements za wasanii wenye umri mdogo” amesema kupitia Planet Bongo ya EATV.

Ameongeza “Nilikuwa naona wana umri mdogo na wameweza kutawala na watu wanatambua vipaji vyao”.

Source : PlanetBongo ya East Africa TV.

## Atulange binti mfalme: Jicho la mwanamke linalewesha

**Na Adam Fungamwango**

WANAUME wamejaaliwa nguvu, lakini ni ukweli usiopingika wanawake wamejaaliwa sana werevu,  ujanja na maarifa.

Mwanaume akitaka lake atatumia nguvu, lakini mwanamke atatumia maarifa zaidi ili kufanikisha. Na hakuna chochote ambacho mwanamke atataka kukifanya kwenye dunia hii cha manufaa yake au familia yake asifanikiwe, kiwe kibaya au kizuri.

Tumesona hata maandiko kwenye vitabu vitakatifu jinsi Eva au Hawa alivyofanya kasheshe kwenye bustani ya Eden, lakini pia Delila, alimvyomfanyia Samson.

Leo tunaiangalia filamu inaitwa ‘Atulange’. Ukiitazama utamjua mwanamke ni mtu wa aina gani. Ni jasiri asiyetumia nguvu.

Imechezwa na Ndayi Abdulaziz, Anyanya Diudonne, One Scholla, Byckson Kidokozi, Theresa Kaindu, Pitchen Pacific,  Fatuma Abongela, Machozi, Simon na Donat Pacific.

Kuna watu wanakufa kwenye himaya na Golami. Anayewaua hajulikani. Mfalme Gobo Gobole anaita walinzi wake watiifu na kuwaambia watafute chanzo, ni nani aliyefanya mauaji hayo.

Baadhi ya walinzi wanatumwa kupeleleza na kurejea na ujumbe kuwa jirani kuna himaya ya mfalme mmoja anaitwa Zangwadi.

Habari zinasema mfalme huyo wa himaya Zingwela, ndiye anayetuma majeshi yake kuvamia raia na lengo lake siku moja kuiteka Golami na kuziunganisha kuwa himaya moja.

Mfalme Gobole anakwenda kwa mtabiri wake ambaye anamwambia katika utabiri wake suala hilo lipo, lakini mwokozi atakuwa ni binti yake, Atulami. Afanye nini? Likawa swali. Mizimu ikatokea na kumwambia mfalme aelekee kwenye himaya ya Zingwela na kila kitu kitafanyika huko. Walinzi walimpeleka binti mfalme mpaka mpakani mwa himaya hizo mbili.

Alipoachwa, walinzi wa  Zingwela waliokuwa kwenye doria walimkuta na kumteka. Wakampeleka kwa mfalme.

Uzuri na urembo wake ulimfanya mfalme Zangwadi asimuulize maswali mengi, ikafuatiwa kumfanya malkia wa pili.

Bifu likaanza baina ya malkia hao wawili. Mkubwa alituma watu wawe wanampeleleza. Kilichomsaidia Atulange hakuwafanya walinzi na wafuasi wa mfalme kama watumwa, badala yake watu wa kawaida wenye haki kama wengine. Hii ilimfanya kupendwa na walinzi, kuliko mwenzake. Ilimsaidia kutekeleza mipango yake akisaidia baadhi ya walinzi wake wa kike kwa siri. Akamuagiza mmoja kwa siri aende Golami kuita majeshi ya kwao ili yaje kuvamia.

Yakafanya kama yalivyoagizwa, wanajeshi wa himaya ya Golami wakaivamia himaya ya Zingwela na kumteka mfalme wao. Mfalme Gobo Gobole anakuja rasmi na kumkamata mfalme mwenzake, akiagiza awekwe jela. Akampongeza binti yake kwa akili nyingi alizotumia. Mfalme anaziunganisha himaya zote mbili zikaitwa Golami.





## Maarifa aacha wosia hadharani

Rapa kutoka Manzese chini ya Madee, Maarifa Bigthinker ameshtua watu baada ta kutoa wosia wake mapema kuwa akifariki akazikwe Kibaha sehemu ambayo yeye anaiwakilisha.

“Niliapa nitafia booth ili baba yangu apate mboga, nawaelewa mtanipata vizuri mkinielewa mtajielewa hamtoipata shughuli niliapa mtoto wa kitaa sitopata sifuri nikifa nikazikwe Kibaha nitaacha nauli”.

Maneno hayo yapo katika moja ya mstari katika ngoma ya maelekezo chapter 2 aliyoshirikishwa na rapa Moni Centrozone pamoja na Rapcha.

## MIKONO YAO HATARI BONGO FLEVA

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa muziki wa bongo fleva hapa nchini umekuwa ukitamba kimataifa. Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo muziki wa kizazi kipya umekuwa ukipendwa na kuheshimiwa sana nje ya mipaka yake.

Wasanii mbalimbali kwa sasa wamekuwa maarufu na wanapiga pesa ndefu kutokana na ngoma zao mbalimbali.

Mwanzo haikuwa rahisi. Muziki wa kizazi kipya ulionekana kuwa ni wa kihuni wakati unaanza kutanua mbawa zake mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kuna watu wanapaswa kupewa heshima zao kwa kuuondoa kuonekana kuwa ni wa kihuni na kuufanya wa heshima kupendwa na hata watu wazima.

Joseph Mbilinyi maarufu kama Sugu na Joseph Haule, Profesa Jay ni moja kati ya wasanii wachache walioigeuza bongo fleva kutoka ilikotoka na kuwa hapa leo ilipo.

Hiyo ni kwa upande wa uimbaji, lakini pia wapo watu nyuma yao, wanaitwa maproduzya. Hawa ni watayarishaji wa muziki.

Ndiyo wanaowatafutia wasanii hao mirindimo kwenye nyimbo zao wanazotambia.

Wakati wa kupigania mapinduzi ya bongo fleva kukiwa na nyimbo za hip hop, R&B, zouk miaka hiyo, wapo maproduzya ambao nao walikuwa na mchango mkubwa kwenye kuifanya tasnia hiyo kukubalika.

**Mika Mwamba**

Jina lake kamili ni Miikka Aleksanteri Kari raia wa Finland. Wasanii na mashabiki wa muziki wanamtambua kama Mika Mwamba.

Anatajwa kuwa ndiye mtayarishaji muziki bora zaidi kwenye muziki wa kizazi kipya. Umaarufu wake ulikuwa mkubwa kuanzia miaka ya 2000, alipowatengenezea ngoma kali wasanii kama Dully Sykes, Inspector Haroun, Lady Jay Dee, Mad Ice, Chegge, Mandojo na Domo Kaya, Solid Ground Family, Complex, Zahrani (maarufu kama Big Punisher wa Bongo), Only Face, Dknob, Daz Nundaz na wengineo.

**P Funk**




Huyu ni mtayarishaji muziki na mmiliki wa Studio ya Bongo Records. Jina lake kamili ni  Paul Matthysse. Ni mmoja wa maproduzya waliowapandisha chati wasanii wengi kama Solo Thang, AY, Zay B, Sista P, Mike T, Ze Pungu, Jay Mo, Chege, Temba, na baadhi ya wasanii wa TMK, pia alishawahi kufanya kazi na Profesa Jay, Afande Sele, Ferouz. Wengine ni Mr II Sugu, Monduli Mobb, Gangwe Mobb, Hop Pot Family ikiongozwa na Soggy Doggy, na Manyema Family.

**Master J**

Anaitwa Joachim Kimario, maarufu kama Master J. Ni mtayarishaji aliyewekeza kwenye studio kadhaa tofauti, na moja ya sifa zake ni kwamba mbali na bongo fleva, lakini pia mtayarishaji wa muziki wa kwaya, pamoja na muziki wa dansi pia. Bendi nyingi za dansi kipindi hicho kama FM Academia, African Stars ‘Twanga Pepeta’, TOT Plus zilikuwa zikienda kurekodi kwenye studio zake, chini yake mwenyewe. Moja ya studio zake maarufu ni MJ Production.

**Henrico**

Ni mmoja wa watayarishaji maarufu wa muziki wa bongo fleva ambaye naye huwezi kumuacha kwenye orodha ya watayarishaji walioibeba tasnia ya muziki wa kizazi kipya, akifanya kazi na wasanii wengi nchini.

Henrico alikuwa kinara studio ya Soundcrafters.

**Said Comorien**

Wasanii wa zamani wa bongo fleva na mashabiki wake hawawezi kumsahau Said Comorien. Alikuwa mtayarishaji muziki alifanya kazi na wasanii mbalimbali, akiwemo Rehema Chalamila, maarufu mama Ray C na wengineo.

Metro Studio, ndiyo alikuwa akiimiliki.

# Mume wa Nicki Minaj jela miaka 3




MUME rapa wa Marekani, Nicki Minaj, amehukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela baada ya kushindwa kujiandikisha kama mhalifu wa vitendo vya kingono.

Kenneth Petty, alihukumiwa siku ya Jumatano, baada ya kukiri mnamo 2021, wakati wa kusikilizwa kwa kesi ya mtandaoni kwa shtaka la kushindwa kujiandikisha kama mhalifu wa ngono huko California.

Petty alikamatwa mwaka 2020 kwa kosa hilo.

Petty alihamia California kutoka New York mnamo Julai 2019, lakini kulingana na utekelezaji wa sheria aliondolewa huko Beverly.



## Eedris aomba dua akifanyiwa upasuaji

RAPA mkongwe wa Nigeria, Eedris Abdulkareem amewasihi wananchi wa Nigeria kumuombea huku akielekea kufanyiwa upandikizaji wa figo.

Katika taarifa iliyotolewa kupitia ukurasa wake wa Instagram, uongozi wa nyota huyo wa muziki ulitoa wito kwa Wanigeria kumuombea katika muda wake wa uchungu.

"Nahitaji maombi ya dhati ya Wanigeria wote na mashabiki wote duniani kote katika saa hizi za uchungu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.


## Paul Okoye siasa ina wenyewe

MWANAMUZIKI wa Nigeria Paul Okoye wa kundi la Psquare, amefichua kuwa sekta pekee inayopiga hatua nchini Nigeria kwa sasa ni burudani.

Nyota huyo wa muziki alifahamisha hayo kupitia ukurasa wake wa Twitter, akisema nchi hiyo iko nyuma kimaendeleo.

"Nigeria iko nyuma kabisa kitu pekee kinachosonga mbele ni muziki/burudani," alitweet.





## Cocker omba yasikukute

MWANDISHI maarufu wa Nigeria, Stephanie Coker amejitokeza kuzungumzia mwenendo wa ndoa za mastaa kushindwa kudumu.

Mrembo ambaye ni mama wa mtoto mmoja, alisema kuanguka kwa ndoa nyingi za mastaa wa muziki ndio zinatangazwa zaidi na kuwatia hofu watu wanaotaka kuingia katika maisha hayo.

"Acheni kutumia ndoa za watu mashuhuri kuwatia hofu watu. Huu ni ujumbe wangu kwa timu ya ndoa yangu itafanya kazi kwa jina la Yesu," ameandika Coker.

## Swift aolewa tena

Mwimbaji wa Marekani Taylor Swift anaripotiwa kuchumbiwa kwa mara nyingine.

Kulingana na PageSix, mwimbaji huyo amechumbiwa na mpenzi wake, Joe Alwyn.

"Kimsingi familia ya karibu, na marafiki wa kuaminiwa, ndio wanafahamu. Kila mtu ameapishwa kutunza siri," chanzo kilifichua.



MAKALA

# Woga na uthubutu unavyoathiri watu kufikia maisha ya mafanikio

Na Mwandishi Wetu



Meneja Masoko na Mahusiano wa UTT AMIS, Daud Mbaga, akitoa maelezo.

UTHUBUTU wa jambo lolote na kusogea hatua moja hadi nyingine, ni changamoto kwenye jamii, haijalishi kundi hilo ni vijana au wazee.

Upo msemo usemao 'Woga wako ndio umaskini wako', dhana hii inaishi miongoni mwa jamii kiasi kwamba fursa zinawapita na kushindwa kukuza uchumi wao.

Mbinu ya kufanikiwa huhitaji wazo, mtaji na rasilimali watu, ndio maana kila uchao vinabuniwa vikundi vya kijamii kama vicoba, vibubu kwa ajili ya kuongeza nguvu ya kifedha na kubuni biashara.

Ingawa baadhi ya vikundi hivyo vinadhoofika kutokana na kutokuwa imara na mfumo wa kuhifadhi mtaji.

Meneja Masoko na Mahusiano UTT AMIS, Daud Mbaga, anazungumzia dhana hiyo kwamba wapo watu ambao ni waoga wa kuwekeza na hufikiri kufanya uwekezaji kwenye mifuko ambayo ni salama sana na faida huwa ya wastani.

"Ili upate faida kubwa ni muhimu kuwekeza sehemu zenye hali hatarishi kidogo. Mfano mifuko inayochanganya hati fungani na hisa. Hisa ni chachu ya faida pia ni chachu ya hasara. Mara nyingi hati fungani zitakupa faida," anasema.

"Mara nyingi maamuzi ya wapi uwekeze yanaendana na malengo, umri, muda na faida tarajiwa. Kwa mfano, mtu anayekaribia kustaafu ataridhika na faida ya wastani," anaongeza kusema Mbaga.

Anasema inatakiwa jamii kubadilika na kuchukua hatua kubadilisha mitazamo.

Anaeleza idadi kubwa ya watu hutamani kuwa matajiri au fedha ziwe nyingi zaidi, ingawa tatizo la woga ndiyo shida kuu.

"Waswahili wanasema woga wako ndiyo umaskini wako. Watanzania wengi hatupendi kuthubutu, tunaogopa. Kumbuka hakuna maajabu duniani, lazima tuwekeze, ili kuongeza kipato chetu.." anasisitiza Mbaga.

Anaongeza kwamba wengi wana pesa zimewekwa nyumbani au benki, bila kufahamu fedha hizo wangezipa thamani zaidi kwa kuziwekeza sehemu salama kama kwenye Mfuko wa Hati Fungani.

Anasema kwa ambao umri umesonga hasa wastaafu hawatapenda kuwekeza sehemu ambayo ni hatarishi kwa kuwa, jambo la kwanza hawana nguvu ya kuhangaika tena ili kutafuta kingine, na alicho nacho kinaweza kuwa turufu yake ya mwisho.

Mbaga anafafanua kwamba jambo hilo ni tofauti kwa vijana ambao wao wanaweza kuthubutu kwa kuwa wana muda wa kuanguka na kusimama, huku wakijifunza kutokana na makosa yao.

"Jifunze kutokana na makosa ya wengine, usisubiri mpaka uanguke ndio ujifunze. Malengo yanaweza kukufanya uwe na msimamo wa woga, mfano mtu anayeweka fedha ili kununua nyumba, ada ya shule ni tofauti na yule anayewekeza ili kwenda kutalii," anasema.

Akazidi kufafanua"Nyumba na ada ya shule ni vitu vya lazima, lakini kutalii si lazima. Pesa ya nyumba na ada ya shule unaweza kuiweka katika hali ambayo si hatarishi sana kuliko utalii unaweza kuiwekeza katika mradi ambao una viashiria vya hatari zaidi ambavyo vikienda sawa vinakupa faida nzuri zaidi,"

Kuhusu mwekezaji mwenye malengo ya muda mrefu, Mbaga anasema kwamba weka fedha sehemu ambayo inampa faida kubwa au ambayo faida tarajiwa ni kubwa, huku dhoruba zake zikiwa juu kama zitatokea.

"Kadri muda na lengo lako linavyokaribia, unaweza kuhamisha uwekezaji katika maeneo yenye hatari za uwekezaji kidogo na faida za wastani. Ili uweze kupata ufanisi ushauri ni muhimu."

Mbaga anasema, Watanzania wengi bado wanaamini benki ndiyo sehemu pekee na sahihi ya kutunza pesa, pia si wote wanaofahamu kwamba benki ni chombo pekee wanachoweza kukitumia kama daraja la uwekezaji.

Anaeleza ni busara kwa mwekezaji kuchukua hatua sasa na kuanza kuwekeza. Kila mtu ana kila sababu ya kuwa mwekezaji, ukiwekeza fedha zako unazipa nafasi ya kukua, hakuna mtu asiyependa kuwa na maisha bora.

"Hakuna mtu asiyependa kuongeza pesa alizonazo, njia bora kabisa ya kuongeza pesa hizo ni kuwekeza kwa makini.Kwa kila tunalofanya tukumbuke kuna maisha ya baadae hasa baada ya kustaafu. ni vizuri ukawekeza kwenye sehemu kama hisa, hati fungani hata kwenye akaunti za muda maalumu," anazidi kusema Mbaga.

Anasema UTT AMIS ina mifuko inayoendana na matakwa ya mteja, ipo yenye mawimbi makubwa, ya kati na madogo. Yote inatoa faida kwa wawekezaji.

Uwekezaji wa aina hiyo ni njia muafaka ya kufanikisha malengo yako kama kununua gari, kujenga nyumba, kuanzisha bishara na kusomesha watoto.

Aidha, Mbaga anasema uzuri wa hati fungani ni kwenye uhusiano wake na uchumi, wakati nchi inataka kuendeleza miradi zaidi inahitaji pesa, pia wakati uchumi unadorora pesa zinahitajika ili kuuweka sawa, hati fungani kila wakati imekuwa kati ya jawabu la



Moja ya huduma inayotolewa na mfuko wa UTT-AMIS ni utoaji mikopo kwa ajili ya kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...



Na Adam Fungamwango

# Kutoka 'pleya', radio kaseti hadi 'sabufa'

## ■Spika iliwekwa kwenye mtungi kupata besi
## ■Kelele marufuku muziki usikike

WATOTO wa siku hizi wana raha sana. Sisi zamani kwenye disco tulikuwa tunacheza kwa sharti la kutopiga kelele. Kwa sababu ukipiga kelele muziki hausikiki, zitasikika kelele tu." Mtangazaji mmoja wa muziki wa zamani kwenye redio moja alisikika.

"Tulikwenda kwenye sherehe moja kwenye shule ya wasichana, tulialikwa sisi wavulana, basi mnacheza huku mnanong'onezana tu, hakuna kuongea kwa sauti kwa sababu vyombo vilivyokuwa vinacheza muziki wakati ule havikuwa na ubora mkubwa kama huu wa sasa. Basi mnacheza kimya kimya, vinasikika viatu tu. Siku hizi mnacheza hata ukipiga kelele unajisumbua. Utaendelea kusikika muziki na siyo wewe mpiga kelele."

Mtangazaji huyo alikuwa sahihi sana. Maisha yanakwenda kasi sana. Hivi sasa disco zinatumia vyombo vingi na vya kisasa. muziki wa disco ukipigwa unaweza kusema kuwa labda kuna dansi linapigwa laivu.

Kwa sasa kuna vyombo ambavyo vinafanya muziki uwe na sauti kubwa zaidi na nzito, kiasi kwamba unaweza hata kukuzibua masikio.

Disco la sasa liwe yumbani au ukumbini kwenye sherehe za kijamii kama, harusi, ubatizo, kipaimara linaweza kupigwa sehemu lakini watu waliokuwa kilometa nyingi mbali wakasikia.

Ni kwa sababu ya teknolojia kuzidi kukua. Kila kukicha wataalamu wanatengeneza vyombo ambavyo vitaufanya muziki uvutie zaidi. Ndiyo maana zamani muziki ulikuwa uko kwenye mfumo wa mono, lakini baadaye wataalam wakatengeneza vifaa ambavyo muziki ukawa unasikika kwenye mfumo wa stereo.





Pleya

Mono ni mfumo wa sauti ambayo inasikika bila kuchujwa. Kama ni muziki unasikika jinsi ulivyo bila sikio kuchambua kama kuna vyombo gani vinapigwa, au sauti.

Mfumo wa stereo inaonyesha sauti iliyochujwa. Wanamuziki wenyewe wana msemo wao kuwa 'imeondolewa mafua.' Sauti ya mono wanaiita yenye mafua. Muziki ukisikika kwa mfumo wa stereo msikilizaji atasikia sauti nyororo, na vyombo vilivyotumika vikijipambanua na kusikika vizuri kabisa.

Wataalam siku zote hawalali. Wakaendelea kuumiza kichwa ndipo walipogundua kuongeza vifaa vya kuongeza sauti kama vile 'booster amplifier', 'subwoofer amplifier', na vingine vingi vinavyofanana na hivyo.

Hata redio za kisasa 'radio subwoofer' maarufu kama 'sabufa' zina sauti kubwa, nzuri, zilizochujwa na mpangilio mzuri wa besi, kiasi cha kuweza hata kuchezesha disco.

Zamani haikuwa hivyo. Ni kweli vyombo vya muziki vilikuwa na sauti, lakini hazikuwa na mfumo mzuri kwenye mpangilio au mfumo wa besi.

Sasa hebu tuhame na kurudi miaka mingi nyuma ambapo watu walipokuwa wakitaka kufanya sherehe za kijamii, iwe za kumaliza shule, chuo, harusi, au disco tu la kawaida.

Achana na zile disco za kwenye kumbi. Nalozungumzia mimi ni lile la mitaani na vijijini.

Mashine moja ya muziki maarufu wakati huo ikiitwa 'record player', maarufu kama 'pleya' ndiyo iliyokuwa inatumika.

Ni kitu mfano wa sanduku ambacho kilikuwa kinazungusha santuri maarufu kama sahani ambayo inakuwa iliyorekodiwa muziki wa aina yoyote ule. Sanduku hilo lilikuwa na spika zake moja au mbili.

Zile spika zilikuwa na sauti,lakini kwa bahati mbaya hazikuwa na besi kutokana na tulichosema huko awali, uduni wa teknolojia.

Kama muziki unasikilizia nyumbani haikuwa na tatizo, lakini kama ni sherehe na hakukuwa na chombo kingine cha kuweza kupiga disco, basi 'pleya' ilifanyiwa utaratibu itoe sauti kubwa zaidi ya ile ya kawaida.

Hapo ndipo utatafutwa mtungi mkubwa, na kile kisanduku cha spika ya kwanza ikawekwa ama juu ya mtungi au ndani, itategemea na mtaalam mwenyewe atakavyoweza kuiseti.

Lengo hapo ni kupata mdundo wa besi ili kunogesha au kupata ladha halisi ya wimbo, pamoja na kuweza kuchezeka kwa raha.

Muziki bila besi ni kama chakula bila chumvi, ndimu, pilipili au kachumbari. Na kweli spika ikiingizwa kwenye mtungi na muziki ukianza kupigwa sauti ya besi inasikika kutokana na sauti ya muziki kuzongwa mtungini.

Kuna 'player' zenye spika moja, lakini pia zipo ambazo zina spika mbili. Sasa hii moja itawekwa kwenye mtungi na nyingine juu ya mti.

Ile inayowekwa juu ya mti lengo lake ni kwamba wote waliokuwa hapo wausikie muziki. Ikikaa chini na kwa vile kuna mkusanyiko wa watu, basi watu wa pande zikingine hawatuusikia vizuri.

Spika inapandishwa juu ya mti, inafungwa, disco linaanza. Sababu nyingine watu wa mbali kidogo nao waonje ladha ya muziki wa kwenye disco hilo.

Hayo ndiyo yalikuwa na mahesabu, ufundi na ujanja na vijana wa miaka ya 1960, 1970, 1980, hadi 1990 mwanzoni.

Hili sasa ndiyo lilikuwa linaitwa 'disco vumbi'. Maana watu kutoka sehemu mbalimbali au vijiji mbalimbali walimiminika kujumuika kwenye sherehe hizo. Wanapotoka hapo ni vumbi tu mtindo mmoja, miguuni, kichwani hadi kwenye kope.

Ilipofika katikati ya miaka ya 1980, taratibu zilianza kuingia, redio kaseti. Na walikuwa nazo watu wachache, hadi katikati ya miaka ya 1990, ndipo zilipoenea mitaani, angalau kwa hata watu wa kipato cha kawaida.

Hapa ndipo yalipokuja mageuzi ya kutoka kwenye 'record player' hadi kwenye redio kaseti.

Na hata mauzo ya santuli yalianza kupungua, kwani watu walinunua kanda za kaseti badala yake. Kila mwenye pesa sasa alitaka kumiliki redio kaseti badala ya 'player'.

Hata hizo redio kaseti zenyewe muda wake ulipokwisha watu waliziweka pembeni na kifaa kinachoitwa 'music system' kilianza kuchukua nafasi yake. Mpaka sasa redio za aina hiyo zipo. Ila 'subwoofer', maarufu kama 'sabufa' nazo kwa sasa zipo kwenye chati.

**Tuma meseji 0716 350534**





Kaseti





Sabufa

HABARI ZA MAONYESHO DITF

# Mkataba wa gesi asilia kutiwa saini Desemba

**Habari zote na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Charles Sangwena, amesema wanatarajia kutia saini mkataba wa nchi hodhi wa kuanza rasmi ujenzi wa mradi wa kuchakata na kusindika Gesi Asilia (LNG) Desemba 8 mwaka huu.

Mkoani Dar es Salaam jana, Sangwena alibainisha kuwa mkataba uliotiwa saini Juni 11 mwaka huu ulikuwa wa makubaliano ya awali na kwamba baada ya hapo kitakachofuata ni usanifu wa mradi pamoja na kukamilisha masuala ya namna ya kupatikana kwa fedha.

Sangwena alisema endapo mambo yatakwenda sawa kama walivyopanga, ujenzi rasmi wa mradi huo utaanza mwaka 2025.

"Kilichotiwa saini Juni 11 mwaka huu kilikuwa ni makubaliano ya awali ya huo mkataba. Tunaendelea kujadiliana na wenzetu na tunategemea Desemba 8 tutatia saini mkataba huu ukiwa umekamilika.

"Pamoja na mkataba huu kukamilika, tunatarajia kwenda kwenye kazi nyingine kama usanifu wa mradi pamoja na kukamilisha masuala ya namna gani tutapata fedha," alifafanua.

Aliongeza: "Tunatarajia kama mambo yataenda yalivyopangwa, ujenzi wa mradi utaanza mwaka 2025. Ujenzi wa mradi mkubwa kama huu ambao thamani yake ni zaidi ya Sh. trilioni 72, unachukua kati ya miaka minne mpaka mitano.

Kwa hiyo, tunategemea mpaka mwaka 2030 gesi ya kwanza, yaani LNG itazalishwa na tutazalisha gesi hiyo kwa kipindi cha miaka 30."

Alisema wazo la Tanzania kuwa na mradi wa aina hiyo lilianza mwaka 2012 baada ya gesi nyingi kugundulika baharini.

"Si mradi ambao umeibuka tu, wazo la mradi huu lilianza tangu miaka ya 2012 baada ya gesi nyingi kugundulika baharini, ulikuja ukasimama hapa katikati kutokana na sababu mbalimbali, lakini kikubwa zaidi ilikuwa ni kushuka kwa bei ya mafuta duniani kuanzia miaka ya 2014 na vilevile kuwapo kwa COVID-19.

"Baada ya serikali ya awamu ya sita kuingia madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya uamuzi mgumu kwamba huu mradi lazima uanze na baada ya kufanya mabadiliko kwenye wizara kuleta waziri mpya, kati ya majukumu aliyopewa kwenye mafuta na gesi, ni kuhakikisha huu mradi unaanza ili gesi ambayo imegundulika kwa kiasi kikubwa kwenye kina kirefu cha bahari ibadilishwe kutoka kwenye hali ya hewa kuwa kwenye kimiminika ili tuibebe kwa wingi kwenye meli kwenda kuuza nchi za mashariki ya mbali kama Japan, India, China na nyinginezo.

"Timu ilichaguliwa mwaka jana Novemba na mimi ndiye mwenyekiti wa majadiliano na timu hii ambayo kazi yake kwa sasa ni kujadiliana na wenzetu ili kuingia mikataba ambayo itaweka makubaliano ya namna ya kutekeleza mradi.

"Na tumeanza na mkataba wa nchi hodhi ambao unaainisha maeneo mbalimbali katika high level.

Kwa hiyo ni mradi ambao unahitaji mipango mizuri kwa sababu utakuwa na manufaa makubwa kwa Watanzania na kwa nchi kwa kuwa kipindi cha ujenzi utazalisha ajira zaidi ya 10,000 na kipindi cha utekelezaji utazalisha ajira kati ya 500 mpaka 600, hizi ni ajira za moja kwa moja kutoka kwenye mradi na sekta nyingine nyingi zitafaidika," alisema.

Kiongozi huyo alisema kutokana na tathmini iliyofanyika miaka ya nyuma, miradi kama hiyo kufanyika kwa nchi kama Tanzania, pato la kitaifa linaongezeka kwa asilimia 1.5 na kwamba matarajio ya mradi ni kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi kwa nchi.




Mshindi wa gari kupitia shindano la Vodacom Tusua Mapene, Abdulrazak Selemani (kulia), mkazi wa Mbagala akionyesha funguo ya gari mpya aina ya Suzuki S Presso baada ya kukabidhiwa katika droo iliyochezeshwa kwenye maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam jana. Wengine ni Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto (katikati) na Mkurugenzi wa kitengo cha Dijitali na Huduma za Ziada Vodacom Tanzania Plc, Nguvu Kamando. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ...TPDC yaahidi mafanikio makubwa katika gesi asilia

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Dk. James Mataragio, amesema yapo matarajio ya kupatikana mafanikio makubwa yatakayotokana na gesi asilia.

Alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonyesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba.

Alisema asilimia 62 ya umeme unatokana na gesi hiyo huku asilia 20 ikitumika katika maeneo ya majumbani na magari.

Mkurugenzi huyo alisema kiasi cha gesi ambacho wamegundua kwa sasa ni futi za ujazo trilioni 57.54 na kwamba kiasi kikubwa cha gesi hiyo kipo baharini ambacho kinatarajiwa kuvunwa.

Alisema mpaka sasa magari zaidi ya 1,500 yameunganishwa na mfumo wa gesi asilia na kwamba karibu kila siku gari moja huunganishwa kwa matumizi ya gesi hiyo. "Kwa hiyo, Watanzania watarajie mafanikio makubwa yanayotokana na gesi asilia," alisema Dk. Mataragio. Alitoa wito kwa sekta binafsi kujitokeza kuwekeza katika sekta hiyo ili kuhakikisha inaleta manufaa makubwa zaidi kwa taifa.

"Sisi tunawahamasisha sekta binafsi wajitokeze kuwekeza katika katika sekta hii na tutawapa idhini kujenga vituo vya kusambaza gesi popote.

"Na wakijenga vituo na vikisambaa inakuwa imerahisisha kwa kuwahudumia wananchi kwa urahisi wanaotumia gesi hiyo eneo lolote," alisema Dk. Mataragio. Alisema matumizi ya gesi asilia pia yanasaidia kuchangia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kwamba ni vyema kuwekeza katika sekta hiyo kutokana na manufaa yake kwa wananchi na kwa taifa kwa ujumla.

# Bodi ya Nafaka yataja tija kilimo cha mkataba

BODI ya Nafaka imesema imeanzisha kilimo cha mkataba na wakulima ambacho kitawasaidia kuendesha shughuli zao hizo kwa tija tofauti na ilivyo sasa.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Dk. Ansezm Moshi, alisema jana kuwa kwa sasa kilimo hicho cha mkataba ni katika soya, ngano na alizeti na kwamba mpango wao ni kuhakikisha mazao yote wakulima wanalima kwa mkataba.

"Tumeshaanza kuendesha kilimo cha mkataba na tumeshaanza kwenye zao la ngano kule kaskazini mkoani Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

"Tunafanya kilimo cha mkataba kwenye soya, na pia kwenye zao la alizeti mikoa ya Singida, Dodoma na Simiyu na mpango ni kuhakikisha kwenye mazao yote wakulima wanalima kwa kilimo cha mkataba.

'Utaratibu wa kilimo cha mkataba, mkulima anakuwa na uhakika na anaunganishwa na benki na mkataba unatiwa saini na taasisi tano, mkulima mwenyewe, benki inayotoa fedha, wanaosambaza pembejeo pamoja na mtu wa bima na hii inasaidia kuwa na kilimo cha tija," alisema.

Aliongeza kuwa kupitia kilimo cha mkataba, wanahakikisha mkulima anakuwa na masoko ya uhakika.

Alisema wakulima ambao wana mikataba mpaka sasa ni 6,000 kwenye maeneo ya kilimo cha ngano, alizeti na maharage ya soya.

"Katika nchi yetu, kilimo cha ngano kilikuwa kimeanguka sana na tukawa hatuzalishi na tukawa tunategemea kwa kiasi kikubwa kuagiza kutoka nje, kwa sasa tuna maelekezo ya serikali ya kuhakikisha tunazalisha ngano ya kutosha Tanzania angalau tufikie tani zaidi ya milioni moja ifikapo mwaka 2025.

"Na ndiyo maana toka mwaka juzi tumetengeneza mikakati hii ya kilimo cha mkataba kwa kuhakikisha, kwanza tunafanya uhamasishaji ili wakulima walime kwa tija na pia wapate mbolea na pembejeo kwa wakati ili wazalishe ngano nyingi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**HAJI KIBABU KHATIB** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2396/0022** kilichotolewa na Baraza La Mitihani la taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI BAMBI mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **KW/RB/3255/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRAYNESS ERNEST LUHWANGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye INDEX NAMBA: **S0203/0039** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia IRINGA GIRLS SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **IRI/IRI/RB/242933/2022**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT
(CAP. 117)**

**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**



**BY THIS DEED, I, LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE of P.O. Box 30112 KIBAHA, DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names of **LAURIAN COSTANTINE MZIBA** and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE.** The reason for the changes of my names is that there was error during registration of my National Identity card bearing number 19900605-61101-00002-23, where the names reads **LAURIAN COSTANTINE MZIBA,** thus it's my wishes my names to reads **LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE** as it appears on my Certificate of Birth attached herein. For the purpose of evidence of such determination, I, hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE** as my name in lieu of and in substitution for my former names of LAURIAN **COSTANTINE MZIBA. AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE. IN WITNESS WHEREOF** I have set my hand at Dar essalaam and I hereon substitute my old names of **LAURIAN COSTANTINE MZIBA** by my new name of **LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE.**

SIGNED and DELIVERED by the said LAURIAN ISHENGOMA COSTANTINE ... DEPONENT

**MAHAKAMA YA WILAYA YA TEMEKE**

**SHAURI LA USIMAMIZI WA MIRATHI Na.196/2022
Katika mirathi ya
ABEL MSAFIRI FUMBO.......................MAREHEMU
NA
EMMANUEL ABEL FUMBO..................MWOMBAJI
(Msimamizi wa mirathi)**

**YAH: MAOMBI KWA WANAOMDAI MAREHEMU-ABEL MSAFIRI FUMBO**

Msimamizi wa mirathi ya marehemu Abel Msafiri Fumbo **(Ndugu Emmanuel Fumbo Abel)** anawakaribisha wale wote wanaomdai marehemu kufika siku ya shauri tarehe 20,Julai,2022,saa 2:30 asubuhi katika mahakama ya wilaya ya Temeke (Dar-es-salaam).
Kwa wale wote wanaomdai marehemu walete ushahidi/kisheria na wafike siku hiyo bila kukosa kwa kuwa orodha ya mali za marehemu zitaorodheshwa na maamuzi yatolewa na kufunga shauri.

JACOB
HM
Juni 2, 2022

## KUPOTEA KADI YA BAJAJI

**GEOFREY ANYITIKE MWAITENGA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **BAJAJI** yenye namba za usajili **MC 184 BZR,** Chassis namba: **MD6M14PA0J419315** Injini namba : **AK4EJ4X24126** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/267483/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**

**KITUO CHA CHAMWINO MKOA WA MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 35...2022**

**JINA LA MDAI: SARAH STEPHANO MAPUNDA**

**JINA LA MDAIWA: BAHATI OMARY**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama ya Mwanzo)**

**KWA: SIKUJUA RAJABU**

**Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba ( Eleza hapo habari za mdai ) MADAI YA PESA YA TSH.847,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 15 mwezi 07 mwaka 2022 saa2.30 Asubuhi kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote zinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shauri, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 05/07/2022.

HAKIMU
MOROGORO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe mjini**

**Mkoa Njombe**

**Usimamizi wa mirathi Na 34/2022**

**Eliezer Bedon Mwakipesile............................Marehemu**

**Renifrida Hongoli..............................................Msimamizi**

**TAARIFA KWA WADAI**

**(Kanuni ya 9(1) ya nyongeza ya V ya sheria ya Mahakimu wa Mahakama sura ya II rejeo la 2019)**

TAARIFA inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu mtajwa hapo juu Eliezer Bedon Mwakipesile aliyefia Hospitali ya Rufaa Njombe, tarehe 24 mwezi Aprili mwaka 2022,na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo Mimi Renifrida Hongoli siku ya tarehe 05 mwezi Julai mwaka 2022,hapa Sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia sanduku langu la barua 54 Njombe au namba ya simu 0737387028 au kuniletea kwa binafsi,ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoisha nitaendelea kukabidhi Mali za marehemu kwa warithi wanaostahili,nikizingatia madai ambayo nitakuwa nimearifiwa.

**Renifrida Hongoli**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.43/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU MWALAMI YUSUPH WA NKUHUNGU
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA KOKOBO MWALAMI YUSUPH**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 02 Mwezi 07 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 12 Mwezi 05 Mwaka 2022

.....................................................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT COMPANY LTD.** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC451CCF,** CHASSIS NAMBA: **LTBPK8BG9J2K06650** na ENGINE NAMBA: **KLL6FMJL8J06650.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/270598/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.92 of 2022**

**In the matter of the Estate of the late of the late FROLA JOHN NDOJE of Nkuhungu within Dodoma Municipality.**

**AND**

**In the matter of application for letters of administration by RUTH NDOJE**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 26 Day of 07, 2022

Dated at Dodoma this 06 day of 07,2022

RESIDENT MAGISTRATE I/C

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.59 of 2022**

**In the matter of the Estate of the late of the late ANDREW BENSON MWAMBOLA of Ihimwa within Dodoma City.**

**AND**

**In the matter of application for letters of administration by ENOCK A. MWAMBOLA.**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12 Day of 08, 2022

Dated at Dodoma this 05 day of 07,2022

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO MJINI**

**Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Shauri la Madai Na.58/2022**

**Jina la Mdai .....................ABDALLAH JOHN**

**Jina la Mdaiwa ............ ISRAEL MWANGWEMBE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni ya taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA. ISRAEL MWANGWEMBE**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
MADAI YA TSH. 2,000,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 29 mwezi 03 mwaka 2022 saa 7:00 mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shihidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
(MCA/84)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MIKUMI**

**Wilaya ya KILOSA**

**MADAI NAMBA ...... 41..... YA......2022**

**MDAI: MIKUMI CREDIT LTD**

**MDAIWA: CHRISANTUS ADRIAN MTANGA**

**MADAI: FEDHA TSH 2,366,665/=**

**KWA: CHRISANTUS ADRIAN MTANGA**

Unaamrishwa na JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 15/07/2022 saa2.30 asubuhi kuwa ni mdaiwa katika shauri lililotajwa hapo juu na ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya mahakama , na unaonywa kwamba ukiwa utapuuza wito huu bila ya udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria

Hati hii inatolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama hii leo 09/06/2022

Kuitwa shaurini hii imetolewa kwa maombi ya **MIKUMI CREDIT LTD**

Hakimu wa Mahakama ya mwanzo







*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# Kama ipo, ipo tu-13

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Hayo yalikuwa maisha ya Sam na wazazi wake, hadi pale baba yake alipofariki dunia miaka miwili iliyopita.

Tangu baba yake afariki, ameweza kutengeneza faida kubwa kwenye biashara aliyoachiwa na baba yake, hivyo utajiri kuongezeka na kuwafanya mama na dada zake kushusha presha kwamba huenda utajiri wao unaweza kuporomoka.

Wakati dada zake ambao ni wadogo zaidi yake walikuwa wameshaolewa, yeye alikuwa bado.

Safari hii hakuna aliyekuwa akimuuliza, si dada zake wala mama yake, walichoangalia wao na kumkubali ni jinsi alivyozibeba biashara za baba yake na kuziendeleza, tena kisomi zaidi kuliko mwanzo.

Akiwa na miaka 27 sasa, akiwa kijana tajiri aliendelea na tabia ile ile ya kutokuwa mlevi, mpenda anasa, badala yake aliendelea kuwa mchapakazi, huruma, upendo, upole na ucheshi.

Akiwa kwenye gari lake la Ranger Rover akisafiri mikoani kwenye shughuli zake za kibiashara alisikia mlio mkali.

Alidhani labda tairi limepasuka. Haikuwa hivyo. Kulikuwa na watu wawili mbele ambao walikuwa wamemuelekezea bastola. Ule mlio aliousikia ulikuwa ni wa bastola ambayo ilikuwa imepigwa juu.

Hakuwa na ujanja, kwani midomo miwili ya bastola ilikuwa imemuelekea, hivyo kama alijifanya kuongeza mwendo basi risasi zile zingepenya kwenye kioo na kummaliza. Akasimama.

Baada ya wale wawili, kumbe kulikuwa na wengine wawili pembeni. Mmoja akamuashiria afungue mlango.

Akatii. Haraka wote waliingia kupitia mlango huo huo. Baadaye wakajigawa, wengine wakakaa siti za nyuma. Mmoja akakaa mbele na Sam.

"Twende hadi tutakapokuambia usimame." Yule wa mbele aliamuru. "Hapana J, usiruhusu huyo aendeshe gari, wewe si unajua kuendesha, mlete nyuma huku halafu wewe endesha." Ilitoka amri kutoka myuma.

Alichomolewa na kuvutwa kwa nyuma. "Jamani kwani mimi nimefanya nini?" Sam akauliza.

Mmoja akacheka halafu akamjibu "Samahani, sisi ni wauaji wa kukodiwa, Tumepewa tu pesa ili tukumalize, kusema sijui umefanya nini hilo hatujui, itabidi tu utusamehe." Alijibu kwa utulivu sana kana kwamba hawana mpango wa kutaka kufanya kitu chochote cha hatari.

**"Yaani we mtoto wewe, hawa dada zako wataolewa, lakini wewe ndiyo mtoto wetu pekee wa kiume, mimi na baba yako tungependa sana kukuona una mtu. Siyo kwamba uoe, hata kumuona tu umekuja naye, umefanya hivi, ili mradi tu mama yako nifurahi na baba yako."**

Wakati huo ilikuwa ni saa 12:00 jioni. Gari iliendeshwa kwa kasi na Sam sasa hakujua wapi anapelekwa kwani alilazwa chini.

Aliamini hivyo kwani hakuwakutaka kuchukua kitu chochote kutoka kwake. Hawakumsachi, wala kuwa na tamaa ya kitu chochote kilichomo ndani ya gari hilo la kifahari.

"Hapo hapo simamisha." Alisikia sauti. Gari liliwekwa pembeni. Walimtoa nje.

"Tumpige risasi?" Mmoja aliuliza.

"Hapana, huyu asipigwe risasi. Kwanza tutashtua watu. Tumekuja huku porini kidogo ili hata kama tukimuua ama askari wachukue siku nyingi kabla ya kuikuta maiti, au iliwe na wanyama wakali na isionekane tena. Kwa hiyo tukipiga risasi, kesho yake tu watu watafika hapa kuangalia tatizo lilikuwa nini?"

"Sawa sasa tumfanyeje?"

"Mpigeni kisawasawa hadi afe. Hapo tutakuwa tumetekeleza lengo letu."

Sam alifungwa kamba na kuanza kupigwa. Hakuweza kujitetea kwa lolote lile. Alipigwa ngumi, vifuti, mateke, makofi, mitama na kila aina ya staili ya mapigo yaliyoingia mwilini bila upinzani wowote.

Alisikia maumivu makali yasiyomithilika, ambayo yalikuwa yakiongezeka kadri muda na mapigo mengine yalivyokuwa yakiongezeka.

Baadaye maumivu yalianza kupungua. Yeye mwenyewe nguvu zikawa zinamuishia. Tayari alikuwa amejikabidhi kwa Mwenyezi Mungu. Hakuwa tena na matumaini ya kuishi. Aliwaza vitu vingi. Aliwawaza dada zake watakavyokuwa wanamtafuta. Akamuwaza mama yake jinsi atakavyokuwa anawahimiza mabinti zake kumtafuta kaka yao.

Sam akawaza jinsi dada zake watakapopata ugumu kuipata maiti yake, kwani pale walipo porini huenda ikaliwa na wanyama wakali.

Akawaza kama wasipomuona kabisa, au kujua kuwa amekufa watakavyolia. Mama yake atalia kwa uchungu kwani tayari amempoteza mumewe. Mume ambaye ndiye alikuwa mmiliki na muongozaji wa mali zote walizonazo.

Kilio chake kilifutika baada ya yeye kuzibeba mali zote. Akaziendesha na kuboresha kila kitu kiasi cha utajiri kuongezeka.

Sam alijua kifo chake kinaweza pia kuwa kifo cha familia yake, mama yake anaweza kufa kwa presha. Aliwaza kama dada zake wanaweza kuhimili mikiki ya kuendesha biashara zilizoachwa na marehemu baba yao mzee Dau.

Aliendelea kuwaza kuwa anakufa bila ya kuwa na mchumba. Mama yake alimsihi sana, lakini alikuwa hataki. Akawaza kama angekuwa na mke au mchumba, huenda angekufa akiwa ameacha mtoto.

"Mwenzetu mkwe ni nani sasa?"

"Mkwe gani?"

"Mchumba, nataka nimuone mkwe wangu kabla sijafa."

Ni maneno ambayo huwa yanamfanya Sam kucheka na kumjibu.

"Naogopa kukuletea, usije ukafa bure mama yangu." Akajibu kwa mzaha.

"Yaani we mtoto wewe, hawa dada zako wataolewa, lakini wewe ndiyo mtoto wetu pekee wa kiume, mimi na baba yako tungependa sana kukuona una mtu. Siyo kwamba uoe, hata kumuona tu umekuja naye, umefanya hivi, ili mradi tu mama yako nifurahi na baba yako."

Sam anacheka tena. Mama yake huwa hamuonei aibu kama wengine.

"Kwani wewe mama una wasiwasi gani? Nikimpata nitamleta tu, ila bado sijampata."

"Au una tabia ya kuchaguachagua, shauri yako, kuchagua kwingi..." Akakumbuka pia maongezi hayo ambayo aliwahi kuongea na mama yake miaka kadhaa iliyopita.

Aliona kabisa kuwa sasa roho yake inakaribia kutoka. Kila kitu sasa alikisikia kwa mbali. Ina maana alikuwa karibuni kuzimia, au kukata roho. Akasikia sauti.

"Basi acha, tuangalie kama amekufa au bado, halafu kama hajafa tummalizie kabisa." Aliisikia sauti hiyo kama yupo kwenye ndoto.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MANULA ATAMANI KUCHEZA UGHAIBUNI, AMSIFIA DIARRA

**Na Shufaa Lyimo**

KIPA chaguo la kwanza wa Simba na Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Aishi Manula amesema anatamani kwenda kucheza soka nje ya nchi kwa sababu ana kiwango na sifa ya kusakata kandanda kimataifa.

Hata hivyo, Manula ambaye alijiunga na Simba akitokea Azam FC alisema bado maslahi kidogo na uhakika wa namba yanakwamisha ndoto zake hizo kutimia. Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Manula alisema kwa kiwango chake anaweza kucheza Rwanda, Burundi, Uganda au Kenya lakini hawezi kwenda huko kwa sababu klabu za huko zinalipa mishahara midogo.

Manula alisema wachezaji wa nchi hizo ndio wanakimbilia Tanzania kwa sababu wanalipwa vizuri ikilinganishwa na kwenye mataifa yao.

"Pia kuna wakati nakumbana na malalamiko kutoka kwa mashabiki pamoja na wapenzi wangu wakidai kwa sasa sistahili kucheza Tanzania kwa sababu kiwango changu ni cha kimataifa.

"Lengo langu ni kwenda nje ya nchi, nataka niende kwenye klabu ambayo inashiriki mashindano ya kimataifa, mashabiki wangu waendelee kuniombea dua ili malengo yangu yatimie," alisema Manula.

Mlinda mlango huyo pia aliipongeza Yanga kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika na kuongeza wamepambana kwa kiasi kikubwa katika kupata mafanikio hayo.

"Ninaipongeza Yanga, wamefanya vizuri msimu huu na ina wachezaji wazuri ambao walijituma na kujitolea mpaka wakafanikiwa kumaliza msimu bila kufungwa," Manula alisema.

Vile vile alimzungumzia mlinda mlango mwenzake kutoka Yanga, Djigui Diarra kuwa ni miongoni mwa magolikipa bora kutokana na uwezo alionao.

"Diarra amefanya kazi nzuri katika kipindi cha msimu huu ambao umemalizika, kila mmoja aliona alichokifanya, ameisaidia timu yake kufikia malengo, pia aliongeza ushindani kwa makipa aliowakuta katika timu yake," alisema mlinda mlango huyo.

Diarra ameshinda tuzo ya golikipa bora kwa msimu uliomalizika lakini pia amekuwa akisaidiwa vyema na kipa namba mbili wa Yanga, Abdultwalib Mshery.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (kushoto), akimkabidhi Tuzo ya Heshima, Kocha Mkuu wa Timu za Taifa za Wanawake, Bakari Shime baada ya kufanikiwa kuipeleka Serengeti Girls katika fainali za Kombe la Dunia (U-17), zitakazofanyika Oktoba, mwaka huu nchini India. **PICHA: TFF**

# CECAFA wanawake yanukia Arusha

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya soka ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa wanawake yamepangwa kufanyika kuanzia Julai 28 hadi Agosti 10, mwaka huu jijini Arusha, imeelezwa.

Vihiga Queens ya Kenya ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya Klabu Bingwa Afrika kwa wanawake.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Auka Gecheo alisema michuano hiyo itakuwa ya mchujo na timu nane zimethibitisha kushiriki.

Gecheo alisema michuano hiyo itachezwa katika viwanja viwili ambavyo ni Sheikh Amri Abeid na Black Rhino Academy uliopo Karatu.

Alizitaja timu zitakazoshiriki ni pamoja na She Corporate FC kutoka Uganda, Yei Joint Stars FC (Sudan Kusini), Warrior Queens (Zanzibar), Fofila PF (Burundi), AS Kigali Women FC (Rwanda), GRFC (Djibouti), Commercial Bank of Ethiopia (Ethiopia) na wenyeji Simba Queens ya Dar es Salaam.

Fainali za Klabu Bingwa Afrika kwa Wanawake mwaka huu zitafanyika Morocco wakati bingwa mtetezi wa michuano hiyo iliyofanyika Misri mwaka jana ni Mamelodi Sundowns Queens ya Afrika Kusini.

Tayari Simba Queens ambayo inanolewa na Sebastian Nkoma, Kocha Bora wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania imeshaingia kambini kujiandaa na michuano hiyo ambapo msimu uliopita ilimaliza katika nafasi ya nne.

## Mgombea Yanga akerwa na bakuli

**Na Shufaa Lyimo**

MGOMBEA wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, Gerald John amesema endapo atafanikiwa kuingia madarakani katika uchaguzi utakaofanyika leo jijini Dar es Salaam atahakikisha mabadiliko yaliyodhamiriwa na kuifanya klabu hiyo kuongozwa kisasa yanafanyika.

John aliliambia gazeti hili amedhamiria kuona ujenzi wa Uwanja wa Kaunda unaomilikiwa na klabu hiyo unakamilika huku pia akipanga kuziendeleza timu za vijana.

"Ninaomba wanachama wa Yanga kesho (leo) wanipe kura zao, ninaahidi kufanya yote ambayo nimeyasema kwenye kampeni zangu nikiwa na lengo la kuifikisha mbali klabu yetu," alisema John.

Aliongeza akiingia madarakani atashirikiana vyema na Rais atakayechaguliwa kuhakikisha timu yao inakuwa bora zaidi lakini pia akiongeza idadi ya wanachama waliosajiliwa rasmi.

"Kwa kuwa klabu yetu ni kubwa hatutaki kutembeza bakuli kama ilivyofanyika siku za nyuma, hii ilinikera sana, tuna uwezo wa kujihudumia wenyewe kama tukiwa na ushirikiano," aliongeza mgombea huyo.

## Sheha, King waula U-17, U-20 Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA wa JKU, Sheha Khamisi ameteuliwa kuwa Kocha Msaidizi wa timu ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Zanzibar (U-17), wakati ile ya U-20 katika nafasi hiyo ameteuliwa, Othman Hassan Omar maarufu kwa jina la King.

Kocha Mkuu wa Timu za Taifa za Vijana Zanzibar, Ali Mohammed Ameir alisema ameteua makocha hao ili kusaidiana naye kuelekea mashindano ya vijana ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika baadaye mwaka huu.

Ameir alisema Kocha wa Makipa wa Malindi, Mbarouk Suleiman Seif, Kocha wa Viungo, Issa Haji Vuai kutoka kitengo cha waamuzi, daktari Haji Makame Ame kutoka KMKM, mtunza vifaa, Khamis Kombo pia wamekuwa sehemu ya benchi la ufundi la timu hizo za vijana.

"Meneja atayeungana na sisi katika kutekeleza majukumu yetu ya kusimamia timu hizi atachaguliwa na ZFF (Shirikisho la Soka Zanzibar," Ameir alisema.

Aliongeza vikosi vya timu hizo mbili za vijana vitatangazwa ifikapo Agosti 15, mwaka huu na baada ya hapo wataanza mapema maandalizi kuelekea michuano hiyo ya vijana itakayosimamiwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NAPOLI YAMTAKA RONALDO
KLABU yaManchester United iko tayari kusikiliza ofa kwa Cristiano Ronaldo msimu huu wa joto huku Chelsea na Napoli wakimtaka mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 37. ***(Sky Sports)***

### LENGLET KUTUA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inakaribia kukamilisha usajili wa beki wa kati wa Barcelona na Ufaransa, Clement Lenglet mwenye umri wa miaka 27, kwa mkataba wa mkopo wa msimu mzima. ***(Standard)***

### AJAX KUIKAMUA UNITED
KLABU ya Manchester United imetakiwa kulipa ada ya uhamisho ya pauni milioni 106 ili kuwasajili mlinzi wa Argentina, Lisandro Martinez mwenye umri wa miaka 24 na winga wa Brazil, Antony (22), wote kutoka Ajax. ***(Daily Record)***

### BRENTFORD VS ERIKSEN
KOCHA wa Brentford, Thomas Frank amesisitiza klabu hiyo ya London Magharibi haikati tamaa katika kumsajili kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30, ambaye anatarajiwa kujiunga na Manchester United. ***(Express)***

### ARSENAL YAMFUATA GRIMALDO
ARSENAL wanafikiria kumnunua beki wa kushoto wa Benfica, Alex Grimaldo mwenye umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAMBANA JAMES
CHELSEA wanatazamia kumpa beki wa pembeni wa England, Reece James mwenye umri wa miaka 22, nyongeza ya mkataba licha ya mkataba wake wa sasa kukamilika Juni 2025, ili kuzuia nia ya Manchester City na Real Madrid kumnasa kirahisi. ***(i Sport)***

### RAPHINHA AENDELEA KUPAA
CHELSEA bado wanapewa nafasi kubwa ya kumsajili Raphinha kwa pauni milioni 55, huku Leeds bado wakisubiri ofa kutoka kwa Barcelona kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 25. ***(Standard)***

### SILVA KUTUA ANDERLECHT
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Fabio Silva mwenye umri wa miaka 19 anatazamiwa kujiunga na Anderlecht kwa mkopo wa msimu mzima kutoka Wolves, ambao walimnunua kwa pauni milioni 35 miaka miwili iliyopita. ***(Mail)***

### LEEDS KUWEKA REKODI
LEEDS United wako tayari kulipa kiasi cha kuvunja rekodi ya klabu cha pauni milioni 31.6 kumsajili mshambuliaji wa Ubelgiji, Charles de Ketelaere kutoka Club Bruges, 21. ***(Mirror)***

### SMITH AGOMBEWA CHAMPS
KIUNGO wa kati wa Arsenal, Matt Smith mwenye umri wa miaka 21 anasakwa na klabu za Championship zikiwamo Millwall na Luton msimu huu wa joto. ***(Sun)***

### GORDON KUTUA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle bado ipo kwenye mazungumzo na Everton kuhusu uwezekano wa kumnunua winga, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21. ***(Chroni-***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAONGEZA OFA KWA MARTINEZ

Lengo ni kushinda vita ya kumsajili nyota huyo ambaye pia anawaniwa na ...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imetuma ofa ya ziada kwa Ajax ili kufanikisha, Lisandro Martinez kutua klabuni hapo, ingawa tayari wana uhakika wa kushinda katika mbio za kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina mbele ya wapinzani wao wa Ligi Kuu Engand, Arsenal.

Kwa mujibu wa 90min ofa ya hivi karibuni United iliwasilisha ofa ya thamani ya karibu euro milioni 50, pamoja na bonasi, huku idadi ya jumla ikifikia hesabu ambayo Ajax ilikuwa imepanga kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Ofa ya awali ya United ilikuwa na thamani ya euro milioni 43, ambayo ilikataliwa.

Martinez ameibuka kama mlengwa mkuu wa safu ya ulinzi ya kocha Ten Hag baada ya United kumkosa mlinzi mwingine wa Ajax, Jurrien Timber ambaye tayari ameithibitishia Ajax nia yake ya kutaka kuihama klabu hiyo kabla ya msimu mpya.

Uamuzi juu ya kukubali zabuni hiyo sasa umeachwa kwa bodi ya usimamizi ya Ajax.

United wana imani matakwa ya wababe hao wa Uholanzi yametimizwa na hivi karibuni na wataweza kukamilisha usajili huo.

Arsenal pia wametoa zaidi ya ofa moja kwa Martinez, lakini bado haijafahamika iwapo watafikia ofa ya hivi United.

Iwe watafanya au la, United "wana imani sana" kwamba raia huyo wa Argentina atachagua kwenda Old Trafford kucheza chini ya Ten Hag kwa mara nyingine.

Vyanzo vimethibitisha kwa 90min, United pia wanaendelea na mazungumzo juu ya Antony, baada ya kubaini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuonyesha nia ya kutaka kutua hapo.

Nyota huyo wa Brazil pia ameweka wazi kwa Ajax angependa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto ili kuchukua changamoto mpya.

90min iliripoti Juni 27, mwaka huu kuwa mabingwa hao wa Uholanzi walikuwa wakitaka angalau euro milioni 120 ili kuwauza wawili hao, ikimaanisha thamani ya Antony hapo awali ilikuwa karibu na euro milioni 70.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,012,7
MECHI KALI
ZENIT ST PETERSBURG
VERSUS
SPARTAK MOSCOW
1 | 1.46
X | 4.21
2 | 5.67
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SUAREZ RASMI AAMUA KUITEMA RIVER PLATE



**BUENOS AIRES, Argentina**

LUIS Suarez amethibitisha hatajiunga na River Plate ya Argentina msimu huu baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini).

90min ilifichua mwezi uliopita kuwa River Plate ilikuwa ikiongoza mbio za kumsajili Suarez, ambaye anapatikana kwa uhamisho wa bure baada ya kumalizika kwa mkataba wake na Atletico Madrid ya Hispania.

Akizungumza na Ovacion, Suarez sasa amekiri uhamisho wake wa kwenda River Plate ulikuwa karibu kukamilika, lakini kuondolewa kwao kwa mshangao kutoka kwa Copa Libertadores kumemaliza matumaini ya klabu hiyo kufikia makubaliano.

"Nilifurahia sana uwezekano wa kwenda River kupigania Copa Libertadores," alieleza.

"Ilikuwa ndoto kwamba nililazimika kushinda Kombe Amerika Kusini. River ilipoondolewa, uwezekano huo umefifia.

"Mwezi mmoja na nusu uliopita nilitamka sitaondoka Ulaya, lakini River ilisisitiza na kusisitiza sana kwamba, nilikuja kulitafakari na kulikuwa na uwezekano."

Kabla ya kumtaka River, Suarez alivutiwa na mchezaji mwenzake wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard huko Aston Villa.

# Bergwijn atua rasmi Ajax

**LONDON, England**

STEVEN Bergwijn amekamilisha uhamisho wake uliosubiriwa kwa muda mrefu na Ajax kutoka Tottenham Hotspur, na kusaini kwa miamba hiyo ya Uholanzi kwa euro milioni 30.

Sakata lake liliendelea katika kipindi chote cha dirisha la usajili la majira ya joto na lilitakiwa na Everton, lakini hivi ilifichuka kwamba, ada ilikuwa imekubaliwa kwa yeye kuuzwa.

Bergwijn alijiunga na klabu hiyo ya Kaskazini mwa London Januari, mwaka 2020 na alianza muda wake mzuri England, akifunga bao lake la kwanza dhidi ya Manchester City katika ushindi wa magoli 2-0.



Hata hivyo, hakuweza kupata nafasi katika kikosi cha kwanza na alifunga mabao nane pekee kwenye michezo 83 aliyocheza ya mashindano yote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alifurahia nyakati za kukumbukwa katika kipindi chake kifupi pale Spurs.

Alifunga bao lao la kwanza dhidi ya Manchester United na akafunga bao lao la kwanza katika mechi ya kichapo dhidi ya Aston Villa.

Timu hiyo ya Amsterdam tayari wamempoteza kocha Erik ten Hag na nyota wa kikosi cha kwanza, Andre Onana, Ryan Gravenberch, Sebastien Haller na Noussair Mazraoui msimu huu wa joto, huku kukiwa na sintofahamu zaidi juu ya hatima ya Lisandro Martinez na Antony.

798,111/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/07/22 | 22:30 | Criciuma SC vs Vasco da Gama | 2.53 | 2.82 | 3.12 |
| 02. 10/07/22 | 00:30 | Sampaio MA vs Ituano SP | 2.47 | 2.98 | 3.03 |
| 03. 10/07/22 | 02:00 | Charlotte FC vs Nashville | 2.45 | 3.22 | 2.97 |
| 04. 10/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs New York Red Bulls | 2.92 | 3.57 | 2.31 |
| 05. 10/07/22 | 02:30 | Goias vs Atletico Pr | 2.89 | 3.08 | 2.54 |
| 06. 10/07/22 | 03:30 | Houston Dynamo vs Dallas | 2.36 | 3.47 | 2.92 |
| 07. 10/07/22 | 08:00 | Consadole Sapporo vs Kashima Antlers | 2.89 | 3.34 | 2.47 |
| 08. 10/07/22 | 13:00 | Sagan Tosu vs Kashiwa Reysol | 2.32 | 3.23 | 3.23 |
| 09. 10/07/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Tokyo Verdy | 2.71 | 3.32 | 2.56 |
| 10. 10/07/22 | 13:00 | Oita Trinita vs Fagiano Okayama | 2.47 | 3.00 | 3.10 |
| 11. 10/07/22 | 13:00 | Avispa Fukuoka vs Kyoto Sanga | 2.62 | 2.97 | 3.02 |
| 12. 10/07/22 | 13:00 | Suwon City vs FC Seoul | 2.90 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 10/07/22 | 16:00 | Utsiktens BK vs Osters IF | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 14. 10/07/22 | 16:00 | Seinajoen JK vs Honka | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 15. 10/07/22 | 19:00 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 16. 10/07/22 | 02:30 | CA Platense vs Newell'S Old Boys | 2.62 | 3.07 | 2.92 |
| 17. 10/07/22 | 22:00 | Corinthians vs Flamengo | 2.73 | 3.08 | 2.68 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 09/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3059 | Daegu vs Ulsan Hyundai | 3.58 | 3.29 | 1.93 |
| 14:00 | 3583 | Taraz Karatau vs Okzhetpes | 4.02 | 3.82 | 1.70 |
| 14:00 | 5609 | Brommapojkarna vs Dalkurd FF | 1.50 | 4.61 | 5.74 |
| 14:30 | 1750 | Shanghai Jiading Huilong vs Tianshan Leopard | 2.55 | 3.24 | 2.50 |
| 16:00 | 1370 | Norrby IF vs Vasteras SK | 1.96 | 3.72 | 3.57 |
| 16:00 | 2627 | Newells Old Boys vs CA Platense | 1.95 | 3.33 | 3.48 |
| 16:00 | 2863 | Malmo vs Varbergs Bois | 1.32 | 4.71 | 7.85 |
| 16:00 | 5290 | Deportivo Maldonado vs Mvo Wanderers | 2.29 | 3.09 | 2.94 |
| 17:00 | 2632 | Ayr United vs Elgin City | 1.28 | 5.11 | 8.25 |
| 17:00 | 2951 | Energetik Bgu Minsk vs Gomel | 2.01 | 3.30 | 3.35 |
| 17:00 | 3068 | Club Guarani De Trinidad vs Sportivo Trinidense | 2.50 | 2.99 | 2.74 |
| 17:00 | 3198 | Hifk vs Haka | 3.88 | 3.34 | 1.84 |
| 17:00 | 3347 | Fraserburgh vs Kilmarnock | 13.80 | 6.90 | 1.13 |
| 17:00 | 3519 | Albion Rovers vs Livingston | 20.62 | 9.23 | 1.06 |
| 17:00 | 3701 | Hibernian vs Clyde | 1.12 | 7.29 | 13.79 |
| 17:00 | 4601 | Bodo Glimt vs Sarpsborg | 1.47 | 4.71 | 5.42 |
| 17:00 | 5227 | Guarani SP vs Cruzeiro | 3.49 | 3.00 | 2.08 |
| 17:00 | 5374 | Dundee FC vs Hamilton | 1.67 | 3.69 | 4.33 |
| 17:30 | 1041 | VPS Vaasa vs IFK Mariehamn | 1.69 | 3.68 | 4.22 |
| 18:30 | 1949 | Lokomotiv Plovdiv vs Pirin Blagoevgrad | 1.54 | 3.84 | 5.31 |
| 18:30 | 2989 | Degerfors vs Norrkoping | 3.20 | 3.54 | 1.98 |
| 19:00 | 2252 | Zenit St Petersburg vs Spartak Moscow | 1.46 | 4.21 | 5.67 |
| 19:00 | 2656 | Vikingur Reykjavik vs IA Akranes | 1.32 | 4.93 | 7.10 |
| 19:00 | 3680 | Patronato Parana vs Arsenal Sarandi | 2.32 | 3.04 | 2.94 |
| 19:00 | 4839 | Stromsgodset vs Odd Ballklubb | 1.85 | 3.81 | 3.66 |
| 19:00 | 5701 | FC Minsk vs BATE Borisov | 5.68 | 4.11 | 1.47 |
| 19:30 | 2888 | CSD Barnechea vs Puerto Montt | 2.50 | 3.09 | 2.65 |
| 19:30 | 4700 | Magallanes vs San Luis Quillota | 1.65 | 3.54 | 4.72 |
| 20:00 | 1273 | New York City vs New England | 1.65 | 4.09 | 4.81 |
| 20:30 | 5405 | CFR Cluj vs Sepsi Osk | 1.94 | 3.19 | 3.67 |
| 21:00 | 1708 | Tristan Suarez vs Estudiantes BA | 3.19 | 2.99 | 2.21 |
| 21:00 | 2526 | Brown Adrogue vs Guillermo Brown | 2.59 | 2.64 | 2.98 |
| 21:00 | 3000 | Mladost Lucani vs Spartak Subotica | 2.25 | 3.10 | 3.20 |
| 21:00 | 3145 | CSKA 1948 vs Levski Sofia | 3.44 | 3.34 | 1.96 |
| 21:00 | 4489 | Javor Ivanjica vs Partizan | 9.40 | 5.29 | 1.24 |
| 21:00 | 4764 | Sporting Cristal vs Sport Huancayo | 1.77 | 3.70 | 4.10 |
| 21:00 | 4945 | Cukaricki St vs Backa Topola | 1.86 | 3.24 | 3.92 |
| 21:00 | 5359 | Dinamo Zagreb vs Hajduk Split | 1.67 | 3.63 | 4.40 |
| 21:00 | 5433 | Club Almagro vs Villa Dalmine | 2.14 | 2.94 | 3.43 |
| 21:10 | 2355 | Lech Poznan vs Rakow Czestochowa | 3.19 | 3.24 | 2.09 |
| 21:30 | 1943 | San Lorenzo vs Boca Juniors | 3.38 | 3.09 | 2.08 |
| 22:00 | 5997 | Curico Unido vs Cobresal | 2.42 | 3.24 | 2.65 |
| 22:30 | 5277 | Bragantino SP vs Avai | 1.59 | 3.62 | 5.09 |
| 23:00 | 4385 | SD Aucas vs Orense SC | 1.73 | 3.58 | 4.12 |
| 23:00 | 5099 | Real Santander vs Llaneros FC | 3.33 | 3.10 | 2.10 |
| 23:00 | 5456 | Tigres FC (COL) vs Fortaleza (COL) | 3.38 | 3.00 | 2.12 |
| 23:00 | 5761 | Leones FC vs Bogota FC | 1.59 | 3.83 | 4.78 |
| 23:15 | 2923 | Envigado FC vs America De Cali | 2.65 | 2.95 | 2.60 |
| 23:15 | 3866 | Ayacucho vs Deportivo Municipal | 1.95 | 3.64 | 3.20 |
| 23:30 | 1408 | Seattle Sounders vs Portland Timbers | 1.88 | 3.72 | 3.87 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# BENKI YA NMB YADHAMINI NETIBOLI DARAJA LA KWANZA

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekabidhi Sh. milioni 10 kwa Chama Cha Netiboli Tanzania (CHANETA) kwa ajili ya kudhamini Ligi Daraja la Kwanza ambayo inatarajiwa kuanza leo kwenye Uwanja Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mgeni rasmi katika uzinduzi wa ligi hiyo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na jumla ya timu 29 kutoka mikoa mbalimbali nchini zitachuana.

Meneja wa NMB Kanda ya Dar es DSalaam, Donatus Richard alisema udhamini huo unaendana na mkakati wa benki hiyo wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) unaosaidia sekta mbalimbali ikiwamo elimu, afya na michezo miongoni mwa sekta yingine.


"Leo tunakabidhi hundi ya Sh. milion 10 ikiwa ni udhamini wetu kwa Ligi Daraja la Kwanza. Udhamini huu kama sehemu ya juhudi zetu za kusaidia maendeleo ya shughuli mbalimbali za michezo. Kama benki, tumekuwa na mchango mkubwa katika kufadhili michezo mbalimbali katika uwanja wa mpira wa miguu na gofu miongoni mwa michezo mingi," alisema Richard.

Aliongeza dhamira ya benki hiyo ni kuendelea kusaidia mipango mbalimbali ya maendeleo ya michezo na kuongeza wanaelewa kwa sasa michezo imegeuka kutoka kwa njia ya mazoezi ya mwili na kuwa njia ya ajira.

Awali, Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa alibainisha kuwa mashindano hayo ni sehemu ya mkakati wa maendeleo wa chama kwa miaka mitano unaolenga kufufua mpira wa netiboli kuanzia ngazi ya chini.

"Mashindano haya ni ya kihistoria kwani yatakutanisha pamoja idadi kubwa ya timu katika historia ya netiboli nchini," alisema Devotha Marwa.

Aliongeza kuwa pamoja na kukuza vipaji vipya, mashindano hayo ni jukwaa la kutafuta wachezaji wa timu ya netiboli ya Twiga Queens.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (wa pili kulia), akimkabidhi Mwenyekiti wa CHANETA, Devotha Marwa, mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya udhamini wa Ligi ya Netiboli Daraja la Kwanza.Kulia ni Meneja Uhusiano wa NMB, Amanda Feruz, na kushoto ni Katibu Mkuu wa CHANETA, Rose Mkisi. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# Coastal Union kupindua meza

**Na Adam Fungawango**

BAADA ya kutajwa imemchukua kiungo mkabaji wao raia wa Nigeria, Victor Akpan, Coastal Union inadaiwa iko katika mazungumzo na beki wa kati wa Simba, Kennedy Juma.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Coastal Union, Ahmed Aurora alisema jana tayari wameshaanza usajili, lakini wao siyo kama timu nyingine zinazotangaza kila hatua waliyofikia, bali wao wanasajili kimya kimya na kwa umakini bila kukurupuka.

Aurora alisema baada ya Abdul Suleimani 'Sopu' aliyejiunga na Azam na Akpan ambaye ameshasaini Simba, nao wameingia katika kinyang'anyiro cha usajili kwa ajili ya kuitengeneza Coastal Union iwe nzuri zaidi kuliko ya msimu uliopita.

Mbali na Kennedy, Coastal Union inatajwa kumwania straika wa Mtibwa Sugar, Jaffar Kibaya pamoja na beki wa kulia wa Prisons, Salum Kimenya.

"Na siyo hao tu peke yao, wapo wengi tumezungumza nao, sitaki kupindisha maneno, ni kweli tunawafuatilia wachezaji wao na kwa asilimia 50 tumemalizana nao, bado tunaendelea asilimia zilizobaki, tukikamilisha tutawatangazia, siku zote sisi hatukurupuki na huwa hatutangazi," alisema Aurora.

Aliongeza kwa mujibu wa mapendekezo ya benchi la ufundi, maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi ni ushambuliaji na mabeki wa pembeni.

# Michezo

Jumamosi Julai 9, 2022

Nipashe




## United yaongeza ofa kwa Martinez




Mkurugenzi Mtendaji Benki ya NBC, Theobald Sabi ( wa pili kushoto), akimkabidhi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mbatha hundi ya mfano ya Sh. milioni 100 kama zawadi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu uliomalizika. Wa tatu kutoka kulia ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa na Rais wa TFF, Wallace Karia. **PICHA: MTANDAO**

# MCHENGERWA ANG'AKA YANGA IKITAWALA TUZO

### ●●●Serikali yafunguka mikakati yapangwa ili Tanzania kuandaa AFCON 2027...

**Na Saada Akida**

WAKATI Yanga ikiendeleza ubabe kwa kutwaa tuzo mbalimbali zilizotolewa kwa waliofanya vizuri katika msimu wa 2021/2022, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa amelitaka Baraza la Michezo Taifa (BMT), kuchukua hatua kali kwa kiongozi yoyote atakayebainika kuvunja maadili ndani ya sekta hiyo.

Mchengerwa alisema hayo kwenye hafla ya utoaji tuzo za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambayo ilifanyika jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Waziri huyo alisema amewataka viongozi wa klabu zote hapa nchini kuzingatia maadili na kuachana na vitendo vya utovu wa nidhamu ambavyo havisaidii kupiga hatua katika maendeleo ya michezo hapa nchini.

"Viongozi wa klabu wanatakiwa kuwa na maadili kwa wenzao, kuna watu wa mpira hawaheshimu viongozi, hili ni jambo la kukemea, nasisitiza BMT kuhakikisha wanawachukulia hatua kali viongozi ambao hawataheshimu wenzao," alisema na aliongeza;

"Viongozi tunatakiwa kuonyesha maadili ili wachezaji wetu huku nyuma wawe na maadili ya kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa, klabu haziwezi kupiga hatua katika michezo endapo hazitazingatia suala hilo,".

"Wenzetu wanafanikiwa sana kwenye michezo kwa kuwa wanazingatia maadili na kuheshimiana wenyewe kwa wenyewe, niwahakikishie wizara ninayoongoza sitakubali kuona mtu wa michezo anakosa maadili na kutoheshimu kiongozi, sitalifumbia macho," alisema Mchengerwa.

Alivitaka vilabu vya michezo kufanya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kujenga miundombini ili kuinua michezo.

"Wakati umefika wa klabu na timu za Tanzania kumiliki viwanja vyao kama ilivyo kwa mataifa mengine huko duniani, naomba BMT na TFF, wiki ijayo ratibuni kikao na viongozi wa vilabu tulimalize suala hili, " alisema waziri huyo.

Aliongeza serikali inatarajia kujenga viwanja vya michezo ya ndani na ukumbi wa sanaa katika eneo la Kawe jijini huku akisisitiza sherehe kama hizo za utoaji tuzo mwakani zitafanyika kwenye ukumbi huo wa kisasa.

Aliongeza dhamira ya serikali kwa sasa ni kuifanya michezo kuwa uchumi na tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya kukarabati viwanja sita ikiwa ni mikakati ya Tanzania kuandaa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), zitakazofanyika mwaka 2027.

"Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa maono yake makubwa ya kuendeleza michezo nchini, serikali imedhamiria kufanya maboresho ya viwanja hivyo kwa ajili ya ya kuomba uenyeji wa AFCON kwa mwaka 2027," Mchengerwa alisema.

Alitaja viwanja sita vitakavyokarabatiwa kwa kuwekewa nyasi za asili ni CCM Kirumba kilichopo jijini Mwanza, Sheikh Amri Abeid (Arusha), CCM Sokoine (Mbeya), CCM Mkwakwani (Tanga), Jamhuri (Dodoma) na Amaan uliopo Zanzibar.

Alisema maboresho hayo ni ya kimkakati na lengo kubwa ni kuona sekta ya michezo inasonga mbele na kuzikumbusha timu kutimiza lengo la kuwa na viwanja vyake.

"Lakini pia wawekezaji na wafanyabiashara huu ndio muda wa kujitokeza kuwekeza katika kuendeleza sekta ya michezo kwa sababu hapo baadae mambo yatakuwa mazuri lakini hamtaweza kupata nafasi ya kuingia kirahisi," alisema waziri huyo.

Bosi huyo wa michezo aliitaka BMT na TFF kuratibu kikao baina yake na watendaji wakuu wa timu zote za Ligi Kuu Tanzania Bara mapema wiki ijayo ili kujadili namna ya utekelezaji wa suala hilo la miundombinu.

Wadhamini wakuu wa Ligi Kuu NBC iliwakabidhi mabingwa wapya wa ligi hiyo, Yanga hundi ya mfano ya Sh. milioni 100 wakati Simba Queens iliyotwaa taji hilo kwa upande wa wanawake ilikabidhiwa kitita cha Sh. milioni 15 kutoka kwa wadhamini wakuu wa ligi yao, Kampuni ya Bia ya Serengeti.

Tuzo ya Mfungaji Bora ilichukuliwa na straika wa Geita Gold FC, George Mpole, aliyetupia mabao 17 wavuni wakati klabu yake ikimaliza msimu katika nafasi ya nne na tuzo ya Mchezaji Bora wa soka la ufukweni ilikwenda kwa Adel Mohamed, Mchezaji Bora wa First League ni Mohamed Hussein na bao bora la msimu wa 2021/22 lilifungwa na Fiston Mayele wa Yanga wakati wakicheza dhidi ya Biashara United.

Tuzo ya Mchezaji Bora wa Kombe la FA ilikwenda kwa Abdul Suleiman 'Sopu' wa Coastal Union huku tuzo ya Mchezaji Bora Ligi ya Wanawake ni Fatuma Maono, 'Fetty Densa' wa Simba Queens na Yannick Bangala wa Yanga alishinda kwa upande wa Ligi Kuu, Meneja Bora wa uwanja ni Sikitu Kilakala wa Azam Complex, Chamazi na Kamishna Bora wa Ligi Kuu ni Abousufian Silia huku ile ya beki bora ikienda kwa Hennock Inonga wa Simba.

Seti ya Waamuzi Bora ni ya mchezo wa Mtibwa Sugar dhidi ya Yanga, ambapo ilichezeshwa na Martina Saanya, Mohamed Mkono, Rashid Gongo na Joachim Akamba na tuzo za heshima za Rais wa TFF, Wallace Karia zilienda kwa Bakari Shime, Stephania Kabumba, Salim Amir na Omar Muhaji (marehemu).

Mwamuzi Bora Msaidizi kwa wanawake ni Glory Tesha kwa Ligi Kuu Bara ni Frank Komba huku wa kati ikienda kwa Ahmed Arajiga, Kocha Bora Ligi Kuu ya Wanawake ni Sebastian Nkoma wa Simba Queens na Nesreddine Nabi wa Yanga alikuwa kwa upande wa Ligi Kuu wakati mchezaji chipukizi kwa wanawake ni Clara Luvanga wa Yanga Princess na kwa Ligi Kuu ni Dickson Mhilu wa Kagera Sugar.

Kipa Bora wa Kombe la FA ni Mohammed Mohammed wa Coastal Union na kwa Ligi ya wanawake ni Gelwa Yona wa Simba Queens wakati kikosi bora cha msimu kinaundwa na Djigui Diarra, Djuma Shaaban, Bakari Mwamnyeto, Yannick Bangala, Feisal Salum na Fiston Mayele, (Yanga), Mohammed Hussein, Inonga na Pape Sakho( Simba), Abdul Suleiman 'Sopu' (Coastal Union) na George Mpole (Geita Gold FC).

## Simba kujichimbia Misri

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kinatarajia kuingia kambini Jumanne tayari kuanza maandalizi ya safari ya kuelekea Misri ili kujiwinda kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Taarifa kutoka Simba inasema kikosi hicho kitaondoka nchini kati ya Julai 14 na 15, mwaka huu na kitaungana na Kocha Mkuu mpya, Zaron Manojlovic jijini Cairo.

Chanzo chetu kilisema katika maandalizi ya safari hiyo, baadhi ya wachezaji jana walienda kufanya vipimo mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Taifa ya Muhimbili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >